# Nipashe

Jumatatu Desemba 4, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581604

nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com


UKURASA WA 3

**Video** ya tabibu kumwagiwa maji tiba yazua balaa

UKURASA WA 4

**Malawi**, Uganda kuitumia kikamilifu Bandari ya Dar



UKURASA WA 17

**Makamu** wa Rais ataka utafiti talaka kuongezeka Z'bar



RASHFORD ATAKIWA KUUNGWA MKONO

UKURASA 22



# Ni maafa

• **Tope** lililobeba magogo, mawe laua; Samia asema yuko njiani kuungana na wananchi... *Endelea ukurasa 2*







Sehemu ya mji wa Katesh wilayani Hanang ukiwa umezungukwa na tope lililotoka katika Mlima Hanang baada ya mvua kubwa kunyesha jana. **PICHA: MTANDAO**

## 49 wauawa na wanyama, nyumba 5,000 kujengwa wanaohama NCAA

UKURASA 19



Rais wa CWT, Leah Ulaya

# Mwalimu ailima barua CWT akipinga kutumia bilioni 7/- kufanya sherehe

UKURASA 19


**MICHEZO** GAMONDI SASA APANIA MEDEAMA UK.24

**KATUNI** UK.6

# Tope la mlima lasababisha maafa

**Na Waandishi Wetu,**
MANYARA

TOPE lililoporomoka kutoka mlimani, limesababisha maafa katika vijiji vinne na Mji wa Katesh, wilayani Hanang', mkoani Manyara, watu 27 wakifariki dunia na wengine 50 wakijeruhiwa.

Maafa hayo yalitokea usiku wa kuamkia jana, wananchi walipozingirwa na maji, tope, magogo na mawe yaliyotokana na mvua kubwa, huku nyumba na magari madogo na makubwa yakizingirwa na tope hilo.

Mwandishi wa habari hizi aliona moja ya mabasi yaliyoegeshwa katika Kituo cha Mabasi Katesh, ambako tope lenye taka nyingi lilionekana likipita huku basi hilo likizingirwa hadi usawa wa nusu ya urefu wake, huku gari la utalii likionekana limejaa tope na magari madogo yakisukumwa.

Taarifa kutoka eneo la tukio zinaeleza kuwa zaidi ya maiti 30 zimeopolewa huku kukiwa na taarifa kuwa vitongoji viwili vimefunikwa na tope hilo.

Vilevile, shughuli za uokozi katika eneo la kusini mwa Mlima Hanang' ambao umezungukwa na Vijiji vya Jorodom, Gendabi, Mogito, Gedan'gonyi na Mji wa Katesh zilikuwa zinaendelea kwa kutumia kamba kuvuta miili ya waathirika toka kwenye nyumba zilizozingirwa na tope hilo.

**KAULI YA RAIS**

Rais Samia Suluhu Hassan alituma salamu za pole, akieleza alikuwa njiani, akirejea nchini kuungana na wananchi kukabili maafa hayo.

Akiwa Dubai, alikohudhuria mkutano wa COP28, Rais Samia alisema ameagiza nguvu zote za serikali zielekezwe katika Mji wa Katesh kwenye uokoaji na kuzuia maafa zaidi kutokea.

Katika taarifa yake, Rais Samia alisema: "Kwa masikitiko makubwa tumepokea taarifa za kutokea kwa mvua kubwa katika Mkoa wa Manyara na kuleta madhara makubwa katika Kijiji cha Katesh.

"Sisi tulioko huku ambao tunashiriki mkutano wa mazingira, tumesikitishwa sana na tukio hili, lakini mipango ya Mungu ndivyo inavyokwenda.

"Mimi na wenzangu tulioko huku tunatoa pole sana kwa waathirika kwa tukio hili, lakini ninataka niseme kwamba, nimeelekeza nguvu zote za serikali zielekezwe huko kwenye uokoaji na kuzuia maafa zaidi kutokea.

"Vyombo vyetu vya ulinzi na usalama tayari nimeelekeza vifike huko, Wizara ya Afya iende kushughulikia majeruhi, lakini pia Wizara ya Madini waende kuona nini kimetokea katika sehemu ambayo milima imeonesha kutetemeka au imeonesha kuporomoka.

"Kwahiyo, nguvu zote za serikali tutatoa huko. Nimemtaka pia waziri anayeshughulika na maafa aweko huko. Sasa ni imani yangu kwamba serikali tukiwako huko basi huduma zinazofaa huko zitakuwa zimebarikiwa.

"Nami niko njiani kurudi kuko kuja kuungana na wananchi katika hili lililotupata. Poleni sana na asanteni sana," alisema Rais Samia.

Wakati hayo yakiendelea, Mkuu wa Kitengo cha Majanga ya Asili wa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania, Gabriel Mbogoni, alisema hatua za haraka zinazopaswa kuchukuliwa ni wananchi kushauriwa kuondoka au kuondolewa kwa nguvu.

Alisema kuwa kwa sasa ni vigumu kutabiri kiwango cha madhara kinachoweza kuendelea kutokea kama mvua itaendelea kunyesha.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi George Katabazi, akizungumza na Nipashe jana, alisema vikosi vya uokoaji vilikuwa vinaendelea na uokoaji ili kusaidia kuwanasua watu waliozingirwa na maji, tope, magogo na mawe yaliyotokana na mvua iliyonyesha usiku wa kuamkia jana.

"Mvua hiyo kubwa iliyonyesha usiku, imesababisha maji kuzingira barabara na hivyo magari yaliyokuwa yanapita Katesh (Hanang') kuelekea Mkoa wa Singida, yamezuiliwa kuendelea na safari mpaka maji yapungue.

"Mpaka sasa (jana mchana), zaidi ya hao watu 27 waliopoteza maisha na 50 kujeruhiwa, hatujajua kama idadi itaongezeka, lakini pia nyumba zilizoharibika bado hazijulikani idadi," alisema.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang', Rose Kamili, ambaye alikuwa kiongozi wa kwanza kutoa taarifa za kuomba msaada kupitia mitandao ya kijamii kwa ajili ya wananchi wa Katesh, alisema hali ni mbaya. Wao, viongozi walikuwa wameshindwa kutoka kwenda kuona maeneo yaliyoharibika.

"Yaani ninakwambia hivi sasa barabara zimekatika, hakupitiki. Sisi tulioko Bassutu, tunatafuta namna ya kwenda kuungana na wenzetu, tunashindwa na walioko Katesh, nao wako wanatafuta namna ya kutoka wanashindwa.

"Kuna watu wamepoteza maisha baada ya kuangukiwa na mawe na miti na nyumba nyingi zimeanguka, ila hazijajulikana ni ngapi, maana waokoaji wanaokota kiungo kimoja kimoja," alidai.

Mkuu wa Wilaya ya Hanang' Janeth Mayanja alisema maji yenye mawe na tope yaliporomoka na kusababisha uharibifu mkubwa miundombinu.

"Ninawapa pole wananchi wa Hanang', vikosi vya ulinzi na usalama vinaendelea na kazi ya kuokoa, Kuna nyumba matope yameingia ndani, hawana pa kulala wala chakala.




"Tutatumia Shule za Sekondari ya Ganana na Kateshi na Shule ya Msingi Dumanani Kata ya Gendabi. Waathirika watahifadhiwa kupata huduma muhimu na wengine wanatibiwa Hospitali za Tumaini na Kateshi.

"Mawasiliano ya Mkoa wa Singida na Manyara yamekatika kwa sababu hapa ndipo pana barabara kuu, lakini TANROADS na TARURA wanaendelea na kazi," alisema.

**WATAALAMU WALONGA**

Akizungumzia maafa hayo, Mkuu wa Kitengo cha Majanga ya Asili wa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST), Gabriel Mbogoni, alisema kwa lugha ya kitaalam kilichotokea kwa ujumla wake, hasa kutiririka kwa tope, mawe na maji, hujulikana kama 'mud flow' na hiyo hutokea hasa zaidi katika maeneo ya miinuko.

"Siwezi kusema ni volcano, kwa sababu sijafika eneo la tukio, na kikubwa zaidi ni mvua inapokuwa inanyesha, udongo umepata maji ya kutosha kwa kiasi cha kutepeta, husababisha udongo kuporomoka na kugeuka tope, hubeba kila kitu kilichoko njiani; taka na vitu vingine vinasombwa.

"Na hali hiyo inachangiwa na shughuli za uharibifu wa mazingira kama kukiwa hakuna miti, miti imekatwa. Kwahiyo, ardhi inakuwa imebaki wazi, vitu kama hivyo ni rahisi kutokea.

"Madhara yake yako kwa uelekeo wa bondeni, ambako maji yanatiririka kuelekea huko, lazima kuna athari kubwa zaidi zikiambatana na vifo," alisema.

Mbogoni alisema, "unajua hayo maeneo ya Hanang' ni maeneo ya Volcano. Kwahiyo, ni maeneo ambayo yalikumbwa na huo mlipuko wa volcano, na majivu yakawa yamesambaa.

"Eneo kubwa limegubikwa na hayo majivu ya Volcano. Yaani udongo wake haujashikamana uko loose (umeachana). Sasa mvua inaponyesha kubwa ni rahisi kusombwa na maji, na ndiyo inatengeneza hilo tope tunaita 'mud flow'.

"Kwa sababu si maeneo tu ya Hanang' na Katesh, lakini Geology ya Tanzania ni 'very unique' (ya kipekee). Kwahiyo, kuna maeneo mengi sana ambayo hayajafanyiwa 'assessment' (tathmini)."

**KWANINI TOPE?**

Mtaalam Mbobezi wa Jiolojia ambaye pia ni Mjumbe wa Bodi ya GST, Dk. Dalali Kafumu, alisema kwa kawaida kwenye jiolojia kuna tabaka la miamba limejipanga, kuna tabaka tope ambalo liko chini, kutokana na mvua zinazonyesha yawezekana maji yaliingia kwenye tabaka hilo na kukawa na mgandamizo uliosababisha tope kupanda juu ya ardhi.

"Tope linaweza kutoka mlimani, lakini la hali ya Hanang' ni eneo la volkano ya zamani, hata mchanga unaweza kutoka chini kama umekosa nafasi kutokana na mgandamizo kisha ukasambaa juu ya ardhi, hivyo eneo hilo lilikuwa na tope, ndilo limetoka," alisema.

Dk. Kafumu ambaye amewahi kuwa Kamishna wa Madini na Mbunge wa zamani wa Igunga (CCM), alisema ni muhimu serikali ikatengeneza utaratibu wa kuyatambua maeneo hayo na kujenga miundombinu muhimu.

"Ninashauri serikali itengeneze utaratibu kwa sababu haikujua kwamba kuna sehemu kama hiyo, kuna sehemu zenye 'mad slide' duniani kama Indonesia ambako wamejnga mitaro mikubwa inayopitisha tope linapojitokeza. Ni mara ya kwanza ninaona hali kama hii kwa eneo la mji kama ilivyotokea Katesh," alisema.

Aliongeza kuwa ikiwa utafiti utafanyika, itasaidia kuyajua maeneo yote yenye hali hiyo na kuwaelimisha wananchi wasijenge au kuwa na shughuli za kibinadamu ili kupunguza madhara, pindi majanga kama hayo yanapojitokeza.

**SAFARI HANANG'**

Kutokana na maafa hayo, serikali imepeleka timu ya wataalamu katika wilaya hiyo ambayo inaongozwa na Mkurugenzi wa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Tanzania, Dk. Ronald Massawe.

Alipoulizwa kuhusu maafa hayo, Dk. Massawe alisema: "Ni kweli niko njiani na timu yangu tunaelekea huko, niko kwenye gari.

Ninadhani baada ya kufika na kufanya geological assessment site (tathimini ya athari za kijiolojia), tunaweza tukaongea kuhusu hilo. Nitafute jioni au kesho nitakupa majibu."

Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) Mkoa wa Manyara, Dutu Masele, akizungumzia madhara katika miundombinu ya barabara na kusababisha kukatika kwa mawasiliano, alisema tayari wamepeleka mitambo, zikiwamo skaveta na katapila kwa ajili ya kuondoa vifusi vya mawe, magogo na tope vilivyofunga barabara ya Babati-Singida.

Shughuli za usafirishaji kupitia barabara kuu ya Babati/Singida zilisitishwa jana kutokana na maafa hayo.

**-Imeandikwa na Godfrey Mushi (ARUSHA) na Jaliwason Jasson (MANYARA): Nyongeza: Salome Kitomari (DAR)**

**HABARI KITAIFA**

# BoT yaonya mawakala, washauri elekezi usajili huduma za fedha

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imeonya kampuni binafsi inayojitangaza kuwa mawakala au washauri elekezi wanaotoa huduma kusaidia waombaji kupata leseni au usajili wa watoa huduma ndogo za fedha kuwa haina utaratibu wa kuwataka waombaji wa leseni au usajili wowote kutumia washauri.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa jana na Kurugenzi ya Usimamizi wa Sekta ya Fedha BoT, imebaini kuwapo taasisi, kampuni na watu binafsi wanaojitangaza kuwa mawakala au washauri elekezi wanaotoa huduma ya kusaidia waombaji kupata leseni au usajili wa watoa huduma ndogo za fedha. Huduma nyingine ni maduka ya kubadilisha fedha za kigeni, benki na taasisi za fedha, watoa huduma za mifumo ya malipo na watoa huduma za fedha kupitia mitandao ya simu zinazosimamiwa na BoT.

"Benki Kuu ya Tanzania inapenda kutarifu umma kwamba haina utaratibu wa kuwataka waombaji wa leseni au usajili wowote kutumia washauri kwenye uandaaji na uwasilishaji wa maombi ya leseni," ilifafanua taarifa hiyo.

Aidha, taarifa hiyo ilibainisha kuwa, BoT imebaini kuwa baadhi ya matangazo yanayotolewa na washauri sio sahihi hasa gharama zinazohusika.

Taarifa hiyo ilisema kuwa BoT inawataka washauri hao kutengenisha gharama za huduma za ushauri na leseni za Benki Kuu kwenye matangazo yao.

Aidha, ilisema kuwa Sheria ya Fedha za Kigeni ya mwaka 1992, Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018 na Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa ya mwaka 2015 na kanuni zake zimeainisha viwango vya mitaji na gharama za maombi ya leseni ya kila aina ya taasisi.

Taarifa hiyo ilibainisha gharama ya maombi ya leseni ambazo hulipwa moja kwa moja katika akaunti ya BoT ni benki na taasisi za fedha Sh. milioni 10 na hakuna ada ya leseni, maduka ya kubadilishia fedha za kigeni Sh. milioni moja na ada ya leseni ni Sh. 500,000 kwa mwaka kwa kila tawi.

Nyingine ni watoa huduma ndogo za fedha (mtu binafsi) ada ya maombi ya leseni ni Sh. 300,000 huku hakuna ada ya leseni; watoa huduma ndogoz a fedha (kampuni), Sh. 500,000 na hakuna malipo ya ada ya leseni.

Wengine ni watoa huduma za mifumo ya malipo ada ya maombi ya leseni ni Sh. milioni moja, na ada ya leseni ni Sh. milioni 12 kwa miaka mitano, huku watoa huduma za fedha kupitia mitandao ya simu wakilipa ada maombi Sh. milioni moja na ada ya leseni Sh. milioni 2 kwa miaka mitano na kwamba malipo hayo yanalipwa moja kwa moja kwenye akaunti ya BoT.

"Benki Kuu ya Tanzania inawakumbusha waombaji wa leseni na umma kwa ujumla kufuata sheria, kanuni na miongozo inayotolewa katika kuandaa na kuwasilisha maombi ya leseni au usajili wa taasisi tajwa ambazo zinasimamiwa na BoT," ilisema taarifa hiyo.

# Video tabibu kumwagiwa maji tiba yazua kasheshe

**Na Vitus Audax**

MGANGA Mfawidhi wa Kituo cha Afya Nyankumbu, Dk. Irene Temba amekana kituo hicho kuwa na watumishi wa afya waliotumia maji tiba 'dripu' kummwagia na kumpongeza mwenzao aliyekuwa akisherehekea siku yake ya kuzaliwa.

Jana asubuhi kulisambazwa kipande cha video katika mitandao ya kijamii kiliwaonesha watumishi wa afya wawili; wa kiume na wa kike wakimwagia dripu mwenzao wa kike, huku wimbo wa pongezi za kuzaliwa siku hiyo, zikisikika.

Ilidaiwa katika kipande hicho cha video kuwa watumishi hao ni Kituo cha Afya Nyankumbu, mkoani Geita.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu jan, Mganga Mfawidhi wa kituo hicho, Dk. Irene, alikana madai hayo, akifafanua kuwa kituo chake hakina watumishi hao na hakina tukio la namna hiyo.

"Hatujajua dhumuni la mtuma video hiyo kukitaja kituo chetu, lakini niuhakikishie umma kuwa watumishi hao si wa kituo chetu na pia mandhari husika hayaendani kabisa na mandhari ya kituo hiki.

"Hivyo, niwaondoe hofu kwani watumishi wetu wana nidhamu, hawawezi kufanya vitendo vya namna hiyo," Dk. Irene alisisitiza.

Alisema kitendo hicho ni kinyume cha maadili ya utumishi wa afya. Anaamini serikali itafanya uchunguzi ili kubaini watumishi hao ni wa kituo gani na kuchukulia hatua stahiki.

Daktari Amon Malanga ni mtumishi katika kituo hicho cha afya. Alipoulizwa na Nipashe kama kuna mtumishi anayemtambua katika kipande hicho, naye alikana. Wanaoonekana katika video si watumishi wenzake.

Alisema, "watumishi hawa sijawahi kuwaona kabisa kituoni kwetu na hatuna manesi wa hivyo. Hata mazingira ya kituo ni tofauti na chetu na hii taarifa si nzuri kwa kituo chetu, lakini tuwaondoe pia wananchi hofu pamoja na wateja wetu waendelee kukiamini kituo chetu na waje kupata huduma," alisema Dk. Malanga.

Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nangu, alinukuliwa na chombo kimoja cha habari jana, akisema, "kutokana na picha hizo kutokuwa na uhalisia wa kituo tajwa, tunaendelea na uchunguzi kujua ni watoa huduma wa kituo gani na tukishapata majibu, tutatoa taarifa kamili."

Hata hivyo, uongozi wa hospitali binafsi ya Sakamu ya mkoani Geita ulitangaza jana jioni kuwa tukio hilo lilifanywa na watumishi wake Desemba Mosi mwaka huu na umewasimamisha kazi.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MRADI WA UENDELEZAJI WA BONDE LA MSIMBAZI**
**(IDA CREDIT NO. 7215-TA)**

## TANGAZO KWA UMMA

### KUSAINI MIKATABA YA MALIPO YA FEDHA ZA KUSAIDIA KUPATA ARDHI MBADALA KWA WATU WANAOATHIRIKA NA MRADI WA UENDELEZAJI WA BONDE LA MSIMBAZI

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) inatekeleza mradi wa uendelezaji wa Bonde la Msimbazi kwa lengo la kukabiliana na mafuriko na kuboresha matumizi ya ardhi katika eneo la chini la bonde. Ili kufanikisha utekelezaji wa mradi, Serikali inatarajia kuwahamisha watu wote wanaoathirika na mradi kwa kuwalipa fidia ya mali zao zinazoathirika.

Serikali, kupitia tamko la Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI la tarehe 15/11/2023, imeamua kuwalipa waathirika wote wanaohamishwa malipo sawa kwa ajili ya kuwasaidia kupata ardhi mbadala. Kampuni ya kusimamia ulipaji wa fidia (PROPERTY MATRIX LIMITED), inayofanya kazi kwa niaba ya OR-TAMISEMI, inatarajia kufanya zoezi la kusainisha mikataba ya malipo sawa kwa ajili ya kupata ardhi mbadala kwa waathirika wote ambao wameafiki malipo yao katika zoezi la mwezi Oktoba 2023. Kampuni hii itafanya zoezi hili katika kila Kata na Mtaa kwa ratiba ifuatayo:

| KATA | MITAA INAYOHUSIKA | TAREHE |
|---|---|---|
| Mchikichini | Msimbazi Bondeni | 6 hadi 7/12/2023 |
| | Misheni Kota<br>Ilala Kota | 8 hadi 9/12/2023 |
| Kariakoo | Kariakoo Kasikazini | |
| Upanga Magharibi | Charambe | 10 hadi 11/12/2023 |
| Jangwani | Mtambani A<br>Mtambani B | |
| Magomeni | Suna | 12 hadi 14/12/2023 |
| Mzimuni | Idrisa<br>Mtambani<br>Mwinyi Mkuu | |
| Kigogo | Kigogo Mbuyuni | 15 hadi 16/12/2023 |
| Hananasifu | Mkunguni A<br>Mkunguni B<br>Hananasifu | |

Wahusika wanaombwa kufika katika maeneo ya usainishwaji wakiwa na vitambulisho (NIDA/Uchaguzi) na nyaraka zote zinazowathibitisha iwapo wanapokea malipo kwa niaba.

**KATIBU MKUU**
**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**



Koplo Stella Mollel, wa Kitengo cha Dawati la Jinsia kituo cha Polisi cha Kawe, akitoa elimu ya utambuzi wa vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi wa shule ya msingi Kawe A katika kuadhimisha siku 16 za kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia yanayoendelea. Jeshi la polisi linaendelea kutoa elimu hiyo kwa shule mbalimbali za msingi na sekondari mkoani Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Malawi, Uganda kuitumia kikamilifu Bandari ya Dar

**Restuta James na Beatrice Shayo**

MABORESHO ya miundombino na kuongeza ufanisi wa bandari yameigusa Malawi, ambayo imetia saini upya mkataba wa kutumia bandari za Tanzania kusafirisha shehena zake.

Waziri wa Uchukuzi na Ujenzi wa Malawi, Jacob Hara pamoja na Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, walitia saini mkataba wa usafirishaji wa ushoroba wa Bandari ya Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

Akizungumza kwenye hafla ya kutia saini iliyofanyika Dar es Salaam, Prof. Mbarawa alisema mkataba huo ulikuwapo siku nyingi, lakini unatiwa saini upya baada ya Tanzania kuwekeza miundombinu ya kisasa kwenye bandari zake.

"Ulikuwapo tangu 1987, sasa tunatia saini upya wakati huu ambao tumejenga miundo ya kisasa na bora (kwa lengo la) kuboresha ushoroba wa usafirishaji baina ya Malawi na Tanzania," alisema.

Aliongeza kuwa serikali imefanya uwekezaji mkubwa kuanzia kujenga gati (lango) namba moja mpaka namba saba na kuweka gati maalum namba zero kwenye Bandari ya Dar es Salaam.

Bandari ya Mtwara imefanyiwa maboresho makubwa kwa kujenga gati ya kisasa lenye urefu wa mita 300 na wiki ijayo serikali itatia saini mkataba wa kuanza ujenzi wa bandari ya kisasa ya Mbamba Bay kwenye Ziwa Nyasa.

"Bandari ya Mbamba Bay ni muhimu kwa sababu ni rahisi kuifikia Bandari ya Mkata Bay iliyoko Malawi na kuziunganisha bandari zetu na Malawi," alisema.

Alisema kujenga na kuboresha miundombinu hiyo kunalenga kuongeza ufanisi na usafirishaji wa kupeleka mizigo huko Malawi, ambayo kwa miaka mingi inaitumia Bandari ya Dar es Salaam.

"Tumetia saini mkataba huu upya ili ufanye kazi vizuri zaidi, wakati huu serikali imejenga miundombinu mingi kuboresha Bandari ya Dar es Salaam na Mtwara lakini pia kujenga meli zitakazosafirisha shehena ya Malawi katika Ziwa Nyasa," alisema.

Meli hizo ni MV Ruvuma, Njombe na MV Mbeya zinazobeba shehena na abiria kwenye Ziwa Nyasa.

Alisema kwa upande wa Malawi usafiri huo utarahisisha usafirishaji na upatikanaji wa bidhaa kwa nchi yao kwa kutumia ushoroba wa Mtwara. Kutapunguza gharama ya usafirishaji na bei za bidhaa.

Aliongeza kuwa pamoja na usafirishaji, serikali imeanza kuleta wawekezaji binafsi kwenye Bandari ya Dar es Salaam na wateja wakiwamo mataifa jirani watarajie ufanisi zaidi kuhudumia shehena.

Akizungumzia faida za ushoroba huo wa usafirishaji, Waziri Mbarawa alisema gharama za uwekezaji kwenye miundombinu zinalipwa kwa kupokea shehena nyingi, hivyo ujio wa mizigo hiyo ni tija kwa taifa.

Waziri huyo alisema ili bandari na reli ziwe na faida, ni muhimu kupokea mizigo kutoka nchi jirani kama vile Congo, Malawi na Zambia ili kupata mapato zaidi.Alisema kuwa mwaka jana, shehena ya Malawi iliyohudumiwa na Tanzania ilifikia tani 553,000 wakati mwaka 2018 ilikuwa tani 300,000 na kwamba ongezeko la mzigo ni muhimu ili kupata faida.

"Kutumia Mtwara Corridor au ushoroba wa usafirishaji wa Mtwara kutapunguza zaidi msongamano kwenye Bandari ya Dar es Salaam," alise,a Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi wa Malawi, Jacob Hara, alipongeza hatua ya serikali ya kuimarisha usafirishaji katika ukanda huo wa kusini mwa Afrika.

Alisema mkataba huo ndiyo ufunguo wa nchi yake kuitumia kikamilifu Bandari ya Dar es Salaam.

Aliishukuru Tanzania kwa kuwezesha biashara na usafirishaji kufanyika kwa ufanisi zaidi na kuahidi wataunganisha reli ya kisasa inayojengwa Malawi na Bandari ya Mbambay upande wa Tanzania ili kuongeza ufanisi. Katika hatua nyingine, Waziri wa Uchukuzi, Prof. Mbarawa na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi wa Uganda, Jenerali Katumba Wamala, wameingia makubaliano kwa ajili ya kuongeza mizigo katika sekta ya usafirishaji ikiwamo kuitumia Bandari ya Dar es Salaam.

Mbarawa aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaama wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kusaini makubaliano hayo, alisema anatamani kuona asimilia 100 ya mizigo ya Uganda inapita Tanzania.

Alisema wamekubaliana kuongeza vifaa kwa ajili ya usafirishaji wa mizigo kwenye reli kwa kuwa wanaamini mikakati hiyo waliyoipanga mizigo itaongezeka hata kufikia asilimia 15 kuliko asilimia mbili ya sasa.

Alisema wataendelea kujipanga na waziri pamoja na wataalamu wake kuhakikisha shoruba ya kusafirisha mizigo kwenda Uganda kupitia Ziwa Victoria na maeneo mengine yatabadilika na kufanya kazi vizuri.

"Tumetembelewa na Waziri Wamala ambaye amekuja kwa madhumuni makubwa kuhakikisha kwamba kwa sasa wanazidisha ushirikiano wa usafirishaji kati ya Serikali ya Uganda na Tanzania hasa kupitia kwenye ushoruba wetu wa Mwanza," alisema Mbarawa.

Alisema anajua kuna makubaliano ya zamani na jana wamefanya mengine kwa ajili ya kuongeza nguvu ya usafirishaji wa mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam kupitia Mwanza na kufika Bandari ya Uganda.

Alisema mizigo kwa sasa inayopita Bandari ya Dar es Salaam ni asilimia mbili kati ya yote ambayo inakwenda nje ya nchi. Asilimia mbili maana yake ni mzigo wenye tani 182,830.

Mbarawa alisema serikali zote mbili zimefanya jitihada kuongeza mizigo kwa asilimia kubwa kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

Pia, miezi miwili iliyopita wamesaini mkataba kwa ajili ya ujenzi wa meli nyingine ambayo itafanya kazi kati ya Mwanza na Bandari ya Uganda na bandari nyingine za Ziwa Victoria.

Waziri Wamala alisema wanatumia ushoroba huo kwa lengo la kuboresha usafirishaji katika utoaji wa huduma bora kupitia Dar es Salaam kwenda Mwanza na kufika nchini Uganda.

Tayari wameshajadiliana na waziri vitu wanavyovitaka kufanyika kupitia ushoruba kuwa hai kwa lengo la kufanya biashara kupitia sekta ya usafirishaji.

Alisema kumekuwa na maboresho makubwa katika Bandari ya Dar es Salaam jambo hilo limewavutia na miundombinu ya usafirishaji ikiwamo ujenzi wa reli ya kisasa kusaidia usafirishaji wa mizigo kwa haraka.

"Mizigo itakuwa inaondoka kwa haraka kutoka bandari ya Dar es Salaam kwenda Mwanza kukamilika kwa reli hiyo ya kisasa ndio maana tumekutana ili kuhakikisha tunakuwa na vifaa vizuri katika usafirishaji wa mizigo," alisema.

# CRDB yapongeza programu ya Rais Samia nishati safi ya kupikia

**Dubai,** UAE

BENKI ya CRDB imepongeza Programu ya Rais Samia Suluhu Hassan ya Kusaidia Nishati Safi ya Kupikia kwa Wanawake wa Afrika (AWCCSP).

Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Abdulmajid Nsekela, ameeleza kufurahishwa kwake na mpango huo, akisisitiza umuhimu wake katika kuwawezesha wanawake na wasichana kote Afrika.

"Kwa kuzingatia maono ya Rais Samia, Benki ya CRDB imejizatiti kuunga mkono mpango huu. Tunatambua nguvu ya mageuzi ya nishati safi YA kupikia katika kuwakomboa wanawake na wasichana kutoka mbinu za jadi za upishi.

"Kama bingwa katika ufadhili wa miradi ya kijani, tuko tayari kutenga fedha mahususi kwa ajili ya nishati safi ya kupikia na kuchangia katika utimilifu wa malengo ya programu," aliahidi Nsekela.

Benki ya CRDB ina rekodi iliyothibitishwa katika ufadhili wa miradi ya kijani, baada ya kutoa Hatifungani ya kwanza na kubwa zaidi ya kijani katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, ikikusanya Sh. bilioni 171.82.

Nsekela alibainisha kuwa fedha hizo zimeelekezwa kwenye miradi rafiki wa mazingira, ikiwamo teknolojia ya nishati safi ya kupikia. Alisema benki ilitenga zaidi ya bilioni 800 mwaka jana kugharamia sekta ya nishati.

"Tunaelewa umuhimu wa kuwawezesha wanawake kifedha, na tuna shauku ya kuunga mkono AWCCSP kuwezesha nishati safi ya kupikia, ipatikane kwa watu wote. Chini ya CRDB Malkia, mpango wetu wa kuwezesha wanawake kifedha (WAFI), tayari tumekopesha zaidi ya Sh. bilioni 600," alibainisha Nsekela.

Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, Tully Mwambapa, pia alipongeza programu ya AWCCSP ya Rais Samia, akiangazia ulinganifu wake na dhamira ya taasisi yao kuwawezesha wanawake na vijana.

"Taasisi yetu imejizatiti kuunga mkono AWCCSP kupitia programu yetu ya IMBEJU, inayolenga kufadhili waanzishaji na masuluhisho ya ubunifu kwa jamii. Nishati safi ya kupikia na ufadhili wa wanawake utapewa kipaumbele katika juhudi zetu," alisema.

Katika miezi minne ya uendeshaji wake, CRDB Bank Foundation imefikia zaidi ya wanawake 100,000 na vijana 709 walioanzisha biashara, wakipatiwa mitaji ya Sh. bilioni tano. Imetolewa kwa wanawake na vijana wanaofanya kazi katika sekta zote.

Kama ushuhuda wa dhamira yake, Benki ya CRDB inashiriki kikamilifu katika COP28 huko Dubai. Ujumbe wa benki hiyo ukiongozwa na Mwenyekiti wa Bodi, Dk. Ally Laay, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Benki hiyo, Prof. Neema Mori na Mjumbe wa Bodi ya CRDB Bank Foundation, Balozi Maulida Hassan, umewahakikishia umma kuwa benki inafanya kazi kuhakikisha sera sahihi zinawekwa ili kusaidia ajenda ya AWCCSP.

Programu hiyo iliyozinduliwa na Rais Samia katika COP28, ni ya miaka mitatu, ikilenga kushughulikia changamoto muhimu za jinsia, mazingira, afya na kiuchumi zinazowakabili wanawake na wasichana barani Afrika kutokana na mbinu za jadi za kupika. Malengo ya programu ni pamoja na kukuza teknolojia ya nishati safi ya kupikia, kuwawezesha wanawake kiuchumi, kuimarisha uwakilishi wa wanawake katika uongozi na kukuza ushirikiano wa kikanda.

Makadirio ya ufadhili unaohitajika kwa ajili ya AWCCSP ni dola bilioni mbili kwa mwaka, ikilenga kupata usaidizi kutoka kwa serikali, ubia wa sekta binafsi, taasisi za hisani na michango.

Mpango huo unalenga kubadilisha maisha ya wanawake na wasichana wa Kiafrika, kukuza teknolojia ya nishati safi ya kupikia, uwezeshaji kiuchumi na uendelevu wa mazingira.

TANGAZO


KILIMANJARO
DRINKING WATER
A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
Mshindi wa
SUPERBRANDS AFRIKA MASHARIKI 2022-2024
VOTED
Superbrands
EAST AFRICA'S CHOICE
2022-2024
Asanteni wateja wetu
Hii ni yetu sote
kilimanjaro_drinking_water
kilimanjarodrinkingwater
kdw@bbl.co.tz
+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga pambaneni, robo fainali inawezekana

**SAFARI** ya wawakilishi wa nchi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika kwa ngazi ya klabu, Simba na Yanga, imeendelea kuwa ngumu tena baada ya kuambualia sare, mwishoni mwa wiki kwenye mechi zao za mzunguko wa pili zilizochezwa juzi, Jumamosi.

Simba ambayo ilianza safari ya michuano hiyo kwa sare ya bao 1-1 nyumbani, Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast, mapema Jumamosi ilipata matokeo ya sare tasa ugenini dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana.

Watani wao wa jadi, Yanga ambao walianza safari ya hatua ya makundi ya michuano hiyo kwa mara ya kwanza baada ya miaka 25, wakikaribishwa kwa kichapo cha mabao 3-0 ugenini nchini Algeria dhidi ya wenyeji wao, CR Belouizdad, Jumamosi usiku wakiwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, waliambualia sare ya bao 1-1 dhidi ya Al Ahly ya Misri.

Kwa ujumla si matokeo mazuri kwa wawakilishi hao wa nchi ambao matarajio yetu makubwa ni kuwaona wakitinga hatua ya robo fainali, nusu fainali hadi fainali kama ilivyokuwa kwa Yanga msimu uliopita wakati ikiiwalisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Matokeo hayo sasa yanaifanya Simba kufikisha pointi mbili katika nafasi ya tatu nyuma ya Jwaneng Galaxy wanaoshika nafasi ya pili ikiwa na pointi nne sawa na vinara Asec Mimosas.

Kwa Yanga matokeo hayo yanaifanya kuambulia pointi moja tu katika mechi mbili ikiburuza mkia katika Kundi D, ambalo Al Ahly ni kinara ikiwa na alama nne ikifuatiwa na Medeama na Belouizdad ambazo zote zina alama tatu kila moja.

Hata hivyo, kimahesabu bado Simba na Yanga, zote zina nafasi ya kuweza kutinga robo fainali na kuendelea endapo tu zitachanga vema karata zao kuelekea mechi zijazo za mzunguko wa kwanza, ambapo safari hii zote zitakuwa ugenini.

Ijumaa Yanga itashuka dimbani nchini Ghana kuvaana na Medeama wakati Jumamosi wiki hii Simba nayo ikiwa nchini Morocco kukipiga dhidi ya Wydad Casablanca ambayo imepoteza mechi zake zote mbili za mwanzo, nyumbani na ugenini dhidi ya Jwaneng Galaxy na Asec Mimosas.

Cha kukumbusha hapa tu, kama msimu uliopita kwenye michuano hiyo, Simba, ilianza kwa kipigo cha bao 1-0 ugenini dhidi ya Horoya ya Guinea, kisha ikarejea nyumbani na kupigwa 3-0 dhidi ya Raja Casablanca ya Morocco, lakini baada ya hapo iliamka na kuanza kutoa vipigo kikiwamo cha karaha kwa kuibugiza Horoya mabao 7-0 kwenye mechi ya marudiano na kutinga robo fainali, kwa nini msimu huu ambao imeanza kwa sare mbili sisi tuikatie tamaa?

Katika hilo, pia linatupa matumaini kwamba nafasi pia bado ipo kwa Yanga, kwani tayari ina alama moja mkononi na imepoteza mchezo mmoja huku ikibakiwa na mechi nne, hivyo hilo linawezekana pia kwao kama juhudi na kiu ya ushindi kwa wawakilishi hao wa nchi itaanzia mechi zao zijazo ugenini na kupata matokeo. Sisi tunaamini mechi zijazo kama wawakilishi hao wa nchi watapata matokeo ugenini njia ya robo fainali itakuwa nyeupe kwao kwani timu wanazokutana nazo, Wydad na Medeama ndizo watakazogeuka nazo kuja kukutana nazo mechi za marudiano kabla ya ratiba kuendelea, ambapo tayari watakuwa wamejenga kujiamini zaidi kutokana na ushindi watakaopata.

Kikubwa kwa Simba na Yanga ni kila mchezaji kutambua thamani ya jezi zao na kuziheshimisha hususan katika mechi zijazo dhidi ya Wydad na Medeama kwa kucheza kufa kupona kuhakikisha wanapata ushindi wao wa kwanza utakaowarejesha ari ya kupambana.

Wakati wachezaji wakiendelea na maandalizi hayo, huu pia ni wakati sahihi kwa mabenchi yao ya ufundi kuwajenga kisaikolojia hasa tukizingatia soka la Afrika lina mambo mengi nje na ndani ya uwanja ambayo kama wachezaji hawakuandaliwa kukabiliana nayo vema, wanaweza kutoka mchezoni na kupoteza pointi muhimu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Adam Fungamwango

### Kila la heri Twiga Stars kufuzu WAFCON mikononi mwenu

**WAKATI** Timu ya Taifa ya soka ya Wanaume, Taifa Stars, ikiwa imeshafuzu kucheza fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2023, zitakazofanyika mwakani nchini Ivory Coast, Tanzania inataka kuweka rekodi nyingine kwa timu ya soka ya wanawake kukata tiketi ya kucheza fainali kama hizo upande wa Wanawake (WAFCON), zinazotarajiwa kufanyika mwakani nchini Morocco.

Itakuwa mara ya kwanza kwa Tanzania kucheza fainali zote mbili kwa wakati mmoja, AFCON kwa wanaume na WAFCON kwa wanawake.

Kama itatokea basi 2024 utakuwa mwaka wa kukumbukwa kwa mara ya kwanza timu za wanaume na wanawake kufanya hivyo, lakini pia 2023 utakumbukwa kwani ndiyo ambao umezipeleka timu hizo hatua hiyo.

Lakini hili litatokea kama kesho Twiga Stars itacheza dakika 90 ikiwa na kazi moja tu ya kuzuia isifungwe mabao 4-0 na Timu ya Taifa ya Togo itakayokuwa nyumbani.

Jumanne iliyopita kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, Twiga Stars iliiadhibu Togo mabao 3-0, hivyo kazi itakayokuwa nayo ni kushinda, kupata sare ya aina yoyote au hata kama ikipoteza isiwe kwa idadi ya kuanzia mabao 4-0 na kuendelea.

Kama Twiga ikiweza 'kushikilia bomba', basi moja kwa moja, timu ya Tanzania kwa wanawake itakuwa imefuzu kucheza fainali hizo mara ya kwanza baada ya miaka 13.

Mara ya kwanza na ya mwisho kwa timu ya wanawake Tanzania, Twiga Stars kucheza fainali hizo ilikuwa ni 2010, zilizofanyika nchini Afrika Kusini ikipangwa Kundi A na ilipoteza mechi zote tatu na timu dhidi ya Nigeria, Afrika Kusini na Mali.

Kocha Mkuu wa Twiga Stars, Bakari Shime, amesema kazi kubwa anayoifanya ni kuwajenga kisaikolojia wachezaji wake kutokana na matokeo mazuri ambayo wameyapata hapa nchini.

Akasema kutokana na kuwa na idadi kubwa ya mabao waliyopata nyumbani, inaweza kuwafanya akinadada hao kuona kama tayari wamemaliza kazi, hivyo kucheza kama tayari wameshafuzu.

Kocha huyo akasema katika mechi hiyo, safu ya ulinzi ndiyo itakuwa mhimili wa kuipeleka Tanzania WAFCON kwani haitakiwi kutetereka.

"Tunakwenda kucheza mechi ya mwisho ambayo itatupa hatma yetu, tumeshinda nyumbani mabao 3-0 hii ni faida kwetu, lakini hatutakiwi kujisahau na kuona tumeshafanikiwa kucheza fainali, kama tutaweka malengo ya kwenda kusaka ushindi ugenini na mabeki wake tuwaweke sawa wacheza bila kufanya makosa yoyote yasiyo ya lazima, tutafanikiwa," alisema Shime.

Binafsi, naiombea kila la heri Timu ya Taifa ya Tanzania ya Wanawake ili nchi iendelee kujiwekea heshima yake kwenye soka ambayo imeanza kujiwekea hivi karibuni.

Tangu uongozi wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), chini ya Wallace Karia, Tanzania imepiga hatua kubwa kwenye maendeleo ya soka, achilia mbali soka la vijana, lakini hata timu za wakubwa, kwani chini yake tu tayari Taifa Stars inakwenda kucheza AFCON kwa mara ya pili ndani ya miaka mitano tu.

Ikumbukwe Stars ilicheza AFCON kwa mara ya kwanza mwaka 2019, ikiwa imepita kiasi miaka 19, tangu ilipofanya hivyo 1980 nchini Nigeria baada ya kufuzu mwaka 1979 kwa kuitoa Zambia. Na katika hali ya kufurahisha, TFF kwa sasa imekuwa ikifanya kazi kwa karibu sana na serikali, kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Baraza na Michezo (BMT), huku Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwa mstari wa mbele kuhakikisha hakuna kitu kinachoharibika, kuanzia kwenye maandalizi, hamasa, miundombinu, usafiri na mengine yanayohusu maendeleo ya soka na michezo mingine pia.

Kwa hayo yote yanayofanyika yameifanya Tanzania kuanza kuwa nchi ya kuogopwa katika soka si kwenye Ukanda wa CECAFA tu, bali Afrika nzima, si kwenye timu za taifa tu hata klabu.

Mwisho niseme tu kila la heri Twiga Stars, pamoja na dua, lakini mnapaswa kupambana kuhakikisha mnafuata nyayo za kaka zenu ambao tayari wana tiketi ya AFCON mkononi.

# Mamalishe wasema nishati safi ya kupikia imewaepushia maradhi

**Na Julieth Mkireri,** RUFIJI

BAADHI ya mamalishe wilayani Rufiji, mkoani Pwani, wamesema matumizi ya nishati safi ya kupikia yanasaidia kuwaweka safi pamoja na mazingira yao ya kupikia tofauti na matumizi ya kuni na mkaa.

Vilevile, wamesema nishati ya gesi inawasaidia kutopata magonjwa ya kifua kwa wanawake na watoto ambayo wanakumbana nayo wanapopika kwa kutumia mkaa na kuni.

Walibainisha hayo juzi walipopokea majiko ya gesi ya kampuni ya ORYX yaliyotolewa na Mbunge wa Rufiji, Mohamed Mchengerwa kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa kampuni hiyo wakati wa Tamasha la Bibi Titi Mohamed lililofanyika Rufiji.

Mwajabu Yassini, mmoja wa wanufaika hao, alisema matumizi ya nishati hiyo mbali na kutunza mazingira, pia yanawarahisishia kufanya kazi zao kwa haraka wakiwa kwenye mazingira safi ambayo hawakumbani na magonjwa ya kifua.

"Ukitumia kuni au mkaa, ukimaliza mazingira yamechafuka na wewe mwenyewe unahitaji usafi ndipo uendelee na kazi nyingine tofauti na gesi. Hii kwetu itatusaidia, tunamshukuru mbunge wetu kwa kutujali," alisema.

Tunu Mkamba, mnufaika mwingine msaada huo, alimshukuru mbunge wao kwa kuwapatia majiko hayo, akiyataja yanaokoa gharama za kununua mkaa. Alibainisha kuwa kwa siku, walikuwa wanalazimika kutumia Sh. 7,000 hadi 8,000 kununua mkaa.

Mbunge Mchengerwa ambaye pia ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), alisema alizungumza na Mkurugenzi wa kampuni ya ORYX kumwelezea uhitaji wa nishati hiyo mbadala ya kupikia kwa wanawake wanaojishughulisha na biashara ya chakula, ili waondokane na matumizi ya kuni na mkaa.

Alisema katika kata 13 mamalishe 13,000 watapatiwa majiko hayo na kwa kuanzia 900 wamepatiwa na watapewa elimu ya kutumia nishati hiyo ili kila mmoja aendelee kutunza mazingira.

Mkurugenzi wa ORYX, Araman Benoit, alisema wanaungana na Rais kuhakikisha wanawake wanatumia nishati safi ya kupikia na kulinda mazingira huku wakiepuka kuvuta moshi mchafu wa kuni na mkaa.

Benoit alisema wananchi wengi wakitumia nishati safi ya kupikia, itawasaidia kuwahisha kuandaa chakula na kuokoa muda kwa watoto na wanawake ambao walikuwa wanatumia muda mwingi kwenda kuokota kuni.

Katika tamasha hilo, mbunge huyo aliomba Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT)kufanya sherehe hizo kila mwaka kwa mikoa tofauti ili jamii imtambue mwasisi huyo mwanamke na wayaige aliyoyafanya wakati wa uhai wake.

# Kampuni yashauri wahandisi wawajibike miradi mibovu

## -Waziri: Kuna uhaba mkubwa wahandisi

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

KATIKA kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan na serikali yake kuimarisha shughuli za uhandisi nchini, Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) imetoa wito kwa sekta ya umma kuweka mpango madhubuti wa usimamizi wa miradi ya ujenzi kuanza hatua za awali za usanifu, ujenzi, kukamilika hadi kutumika kwake ili miradi hiyo idumu kwa muda mrefu.

Pia imetoa ushauri kwamba kuwapo uwajibikaji kwa wahandisi pindi wanaposhindwa kusimamia misingi ya taaluma yao katika masuala hayo ya ujenzi ili kuimarisha shughuli za kihandisi kwa upande wa sekta ya umma.



Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa.

Ni rai iliyotolewa mwishoni mwa wiki na Mhandisi wa kampuni hiyo anayedhibiti ubora na viwango vya miradi, Maftah Seif alipochangia mada katika Kongamano la Kitaifa la 32 la Taasisi ya Wahandisi Tanzania lililofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC).

Seif alikuwa anachangia mada kuhusu sababu za kitengo cha matengenezo kwenye miradi inayohusu ujenzi wa mitambo na majengo katika sekta ya umma kudorora ilhali kwenye sekta binafsi inadumu kwa muda mrefu.

"Tunashauri kwanza kuwe na mpango mzuri kuanzia mradi unapoandaliwa, unapojengwa, unapomalizika na kwenda kwenye hatua za operesheni (matumizi) kwamba kuwe na namna kuusimamia. "Kwa mfano, mradi unapojengwa, ukikamilika lazima kuwe na gharama za kuuendesha kwa sababu mradi unaishi. Hivyo, lazima kuwe na gharama za matengenezo.

"GGML tunaamini mradi hauwezi kufa bila kujua, ndio maana pia tunatoa ushauri kwenye maeneo makubwa mawili kwani dunia imehama kutoka utamaduni wa kawaida na kuwa na wabobezi wanaojua kutumia teknolojia mbalimbali," alisema.

Seif ambaye alikuwa mmoja wa wahandisi 16 walioshiriki kongamano hilo kutoka GGML, alisema ili kufanikisha mabadiliko hayo kwa upande wa sekta ya umma, lazima kuwe na rasilimali watu.

"Lakini pia kuwe na uwajibikaji hasa kwetu wahandisi, tuondoke kwenye utamaduni wa kufanya kazi kwa mazoea, kuwe na idara inayompima na kumbana mhandisi husika anapokiuka vigezo vya mradi badala ya kuubana uongozi wa juu ambao hauhusiki moja kwa moja," alisema.

Awali akizungumza katika kongamano hilo, Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa aliiagiza Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) kushirikiana na Taasisi ya Wahandisi Tanzania (IET) kuweka utaratibu endelevu wa kuwajengea uwezo wahandisi ili waendane na mabadiliko ya teknolojia.

Akifungua kongamano hilo kwa niaba ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Waziri Bashungwa alisema mhandisi ni mwanafunzi maisha yake yote, hivyo aliwaagiza ERB wakiungwa mkono na IET, kuweka mpango maalum wa kuwapatia ujuzi wahandisi walioko kazini kwa kutumia miradi iliyopo.

Bashungwa pia aliagiza ERB kupitia upya vigezo vya usajili wa wahandisi kwa kufungua milango na kuondoa vikwazo visivyo vya lazima katika usajili.

"Idadi ya wahandisi mahiri inatakiwa kuwa mhandisi mmoja kati ya wananchi 5,000. Kwa hesabu za haraka, tunatakiwa kuwa na wahandisi mahiri zaidi ya 12,000, lakini nimeambiwa wahandisi washauri elekezi ni chini ya 500," alisema.

Bashungwa alisema azma ya serikali ni kujenga uchumi ulio imara ndio maana imejielekeza kwa kiwango kikubwa kujenga uwezo, juhudi, maarifa, weledi, nidhamu, umakini na ufanisi kwa wataalamu hao.

Waziri Bashungwa pia aliipongeza GGML na kuipatia zawadi ya cheti kwa kutambua mchango wa kampuni hiyo katika kuwezesha kongamano hilo pamoja na ushiriki wake.


**COMPREHENSIVE COMMUNITY BASED REHABILITATION IN TANZANIA (CCBRT)**

**TAARIFA KWA UMMA**



*Bw. Thomas Geredina Mkinga*

Hospital ya **CCBRT** inapenda kuutarifu umma kwamba **Bw. Thomas Geredina Mkinga,** ambaye picha yake inaonekana hapo juu sio mfanyakazi wa **CCBRT** kuanzia Tarehe **1 Novemba 2023.** Hivyo **CCBRT** haitahusika kwa namna yeyote na makubaliano au shughuli zozote zitakazofanywa na mtajwa hapo juu zikihusisha **CCBRT.**

2177739002



**DAR ES SALAAM CITY COUNCIL**

**PUBLIC NOTICE**

The Dar es salaam City Council is hereby informing all parties interested of that Land, we have received the application for issuing of a right of occupancy on Plot No. 395 Block 'A' KIPAWA AREA from SALEHE KIONDA transfer to ISMAIL SALUM MINTANGA (Legal Personal Representative) of YUSUPH SALUM MITANGA (deceased) of P.O. Box DAR ES SALAAM. By this notice you are given Thirty days (30) to inform City Council director if there is any court injunction, cases, disputes or appeal, otherwise the application will be accepted according to the law.

*Farida Ramadhan Chambulilo*
For: CITY DIRECTOR
DAR ES SALAAM CITY COUNCIL



**KUPOTEA KWA VYETI**



**EMMANUEL D. MKINGA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0179-0007** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ST. MARY'S SEMINARY MBALIZI** mwaka 2007 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0121-0508** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ST. JAMES SEMINARY** mwaka 2010. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/UBU/28641/2023.**



**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya DODOMA MJINI**
**Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**
**Shauri la Madai Na 314/2023**
**Jina la Mdai GLORIA EUSTACE RUBANDWA- DODOMA MJINI**
**Jina la Mdaiwa KCT MOTORS COMPANY LTO-DAR ES SALAAM**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa KCT MOTORS COMPANY LTD- DAR ES SALAAM**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/ Wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai) MADAI **T.SHS 6,800,000/=** Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii JUMATANO tarehe 06 Mwezi 12 2023 saa 2.30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku tajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini. Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 01 Mwezi 12 Mwaka 2023

HAKIMU

1177739202

# Waraibu wapewa elimu waachane na matumizi ya dawa za kulevya

**Na Zanura Mollel**

WARAIBU zaidi ya 150 Kanda ya Kaskazini wamepatiwa elimu kuhusu madhara ya matumizi ya dawa za kulevya na kutakiwa kuacha kuendelea kutumia dawa hizo zilizobainika kupoteza nguvukazi ya taifa.

Mafunzo hayo ni mwendelezo wa mafunzo mbalimbali yanayotolewa katika maeneo mbalimbali nchini na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA). Kwa Kanda ya Kaskazini, yalifanyika mwishoni mwa wiki katika Chuo cha Ufundi Arusha (ATC).

Ofisa Msimamizi wa Elimu wa DCEA Kanda ya Kaskazini, Shaban Miraji alisema lengo la mafunzo hayo ni kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya nchini na kuwaasa waraibu hao kutoendelea kujihusisha na biashara na matumizi ya dawa hizo.

"Elimu hii tumeileta kwenu kutokana na mikoa ya Kanda ya Kaskazini ambayo ni Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Manyara kuonekana kuongoza kwa matumizi ya dawa za kulevya aina ya bangi na mirungi," alisema.

Miraji alieleza kuwa katika kipindi cha kuanzia Septemba hadi Novemba mwaka huu, mamlaka ilikamata magunia 316 ya bangi pamoja na mbegu kilo 130 kwenye operesheni iliyofanyika Kanda ya Kaskazini.

"Mamlaka imetoa elimu vyuoni, shule za msingi na sekondari kwa lengo la kuwaandaa wanafunzi kutojihushisha na matumizi ya dawa hizo," alisema.

Miraji alisema DCEA imebaini baadhi ya waraibu katika kanda hiyo hawajaanza kujitokeza kupata matibabu licha ya serikali kusogeza huduma hizo kwao. Kanda hiyo ina vituo viwili vilivyoko Arusha na Tanga. "Kuna vituo 16 nchini, nyumba za kuhudumia waraibu zaidi ya 53 na kwa Kanda ya Kaskazini pekee zipo nyumba 24," alisema.

Miraji alisema mamlaka hiyo imejipanga kuendelea kutoa elimu kupitia majukwaa mbalimbali ikiwamo sekta ya sanaa ambayo imeonekana ndio kundi kubwa linalowafikia vijana kwa haraka. "Wale waliobanika kuwa na vipaji tutawaendeleza ili waweze kuachana na matumizi ya dawa hizo. Tumebaini kuwa dawa za kemikali zinaharibu meno kwa kuozesha na watumiaji wa mirungi wanaua ini. "Hivyo, nitoe rai kwa watumiaji wa mirungi kuacha, hususani madereva wa malori ya masafa marefu kwani utumiaji wake unachangia ongezeko la wagonjwa wa bawasiri," alionya.

Naomi Massawe ni miongoni mwa waraibu waliopata mafunzo. Alibainisha alitumia dawa za kulevya kwa miaka mitano. Alianza wakati anajishughulisha na kazi ya uchimbaji madini katika mji mdogo wa Mirerani, mkoani Manyara.

"Kwa sasa nina miaka miwili toka nimeacha kutumia dawa hizo. Ninajihusisha na masuala ya ususi. Changamoto nikisuka, ninapewa fedha kidogo ambazo haikizi mahitaji yangu.

"Niliacha dawa hizi baada ya mtoto wangu kutoridhika na matendo yangu, pia nilitambua hazina faida kwenye maisha yangu," alisema Naomi.

Mkuu wa Idara ya Afya Kitengo cha Dawa ya Methodone katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Arusha (Mount Meru), Dk. Said Salum alisema huduma za matibabu kwa waraibu wa dawa za kulevya ni bure, hivyo aliwataka kufika katika vituo vilivyotengwa kupatiwa matibabu.

DCEA imetoa mafunzo kwa kushirikana na asasi mbalimbali zikiwamo Kimara Peer, Care for All, YOVARIBE, YCR, Mount Meru Sober House, Ofisi ya Ustawi wa Jamii Arusha, Ofisi ya Mganga Mkuu Arusha, Mratibu wa Afya ya Akili Arusha, Msimamizi wa Mount Meru Clinic na vyombo vya habari.

# Wanaume waitwa washiriki vita dhidi ya ukatili kijinsia

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF) kwa kushirikiana na Mtandao wa Kupinga Ukatili wa Kijinsia (MKUKI), wamewaomba wanaume na vijana kushiriki katika mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia.

Mratibu wa Kitaifa wa WiLDAF, Anna Kulaya, alisema mwishoni mwa wiki kuwa kundi la wanaume ni muhimu katika mapambano hayo kwa kuwa ndilo limekuwa mstari wa mbele kushikilia mila na desturi kandamizi zinazochangia vitendo hivyo.

"Na wao ni rahisi sana kufahamu viashiria vya ukatili ikiwamo ubakaji, ulawiti na wengi wao ndio wenye mamlaka ya kukataa kuoa watoto wenye umri mdogo na wana wajibu mkubwa wa kulinda wanawake na watoto.

"Kwahiyo, ushiriki wao katika mapambano dhidi ya vita hivi; mimba za utotoni, ndoa za utotoni, ukeketaji na ubakaji utazuilika," alisema Anna.

Alisema vitendo vingi vya ukatili ambavyo vimekuwa vinaripotiwa katika vyombo mbalimbali za sheria, wahusika wakubwa wa kutenda vitendo hivyo ni wanaume.

Alisema katika kipindi hiki cha Siku 16 za Uanaharaki wa Kupinga Ukatili wa Kijinsia, wanafanya kampeni ya kupita mikoa mbalimbali kutoa elimu ya kupambana na vitendo hivyo.

Miongoni mwa makundi yanayozingatiwa katika elimu hiyo ni wanaume na vijana.

"Na kanuni kubwa tunayoituimia mwaka huu tunasema hatumwachi mtu nyuma na inalenga kufika chini kabisa kwenye shina, tukihamasisha watu kuchukua hatua ya kuvikataa vitendo hivyo na kushirikiana kuvikomesha," alisema Anna.

Mmoja wa wadau wa kupinga ukatili wa kijinsia kutoka Mwananyamala, Dar es Salaam, Gerard Kamugisha, alisema miongoni mwa changamoto wanazokutana nazo wakati wa kufanya kazi hizo za kusaidia watu waliofanyiwa ukatili ni familia kumalizana na watuhumiwa.

"Na hili ndilo linatukwamisha sana, tunajitahidi sana kuwaelimisha kwamba hicho wanachofanya kukubaliana kulipwa kitu kidogo na watuhumiwa halafu wakataa kutoa ushirikiano wa vyombo vya dola, ni hatari," alisema.


SIMBA CEMENT
STRENGTH WITHIN

## INVITATION FOR TENDERS FOR SERVICES

1. Tanga Cement Public Limited Company is hereby soliciting bids from interested eligible companies and individuals to supply spares and render services listed in the schedule below.
2. Interested eligible bidders may obtain a complete set of bidding documents from the office of the Procurement Manager located at the Tanga Cement premises in Tanga between 08H00 and 14H00 Mondays to Fridays (excluding public holidays).
3. Sealed bids must be deposited in the Tender Box located at the Tanga Cement visitors' gate in Tanga by 12H00 on the **18 December 2023.**
4. Sealed tenders and modifications thereof must be deposited in the Tender Box located at the visitors' gate by 12H00 noon on the closing date indicated above. All tenders submitted must remain valid for **the period specified in the tender documents** from the closing date indicated above. All tenders must be sealed, marked with the **relevant correct tender title** and addressed to:

**The Managing Director**
**Tanga Cement PLC**
**P O Box 5053**
**Tanga**
**Tanzania**

5. This invitation to bids it does not in constitute an offer to a contract or bind the Company in any way.
6. The bidding documents will be purchased by interested bidders and collected at Tanga Cement office or by email upon payment of non-refundable fee of **Tanzanian Shilling (TZS) 100,000.00 (one hundred thousand)** through either of the below bank details.

| Bank Name | Account number | Account Name |
|---|---|---|
| CRDB Bank | 0150385602300 | Tanga Cement PLC |
| NMB Bank | 41710039344 | Tanga Cement PLC |

7. Tanga Cement is not bound to accept the lowest or any other bid.
8. All bidders must have the approved relevant level of ***"local content"*** as required by the Mining Commission

| S/N | Tender number | Tender Tittle | Comment |
|---|---|---|---|
| 1 | TCPLC-11-2023 | Hiring of Earthmoving Equipment for Mining Operations at Holili Pozzolana Quarry | 2 years contract commencing 01/01/2024 |
| 2 | TCPLC-12-2023 | Provision of Staff transportation Services | 2 years contract commencing 01/02/2024 |
| 3 | TCPLC-13-2023 | Supply of Bearings | 2 years contract under Vendor Managed Inventory **(VMI),** commencing 01/02/2024 |


# Wizara yaweka mkakati kuzuia maambukizi VVU

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WIZARA ya Afya imeweka mkakati kusaidia makundi yakiwamo ya vijana na wanawake kukabiliana na maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU) ikiwamo kuanzisha mafunzo ya malezi kwa wazazi na vijana.

Mratibu wa Huduma za Vijana Wizara ya Afya -Mpango wa Kudhibiti Ukimwi na Magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini (NASHCoP), Patricia Kuya alibainisha hayo mwishoni mwa wiki alipozungumza na mwandishi wa habari kwenye banda lao wakati wa maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika kitaifa mjini hapa.

Alisema mipango hiyo imezingatiwa baada ya kuona kuna pengo kwenye jamii kutokana na wazazi kutoongea na vijana wao kuhusu masuala ya afya ya uzazi hususani masuala ya Ukimwi, mimba za utotoni na magonjwa ya ngono.

"Kupitia mpango huu, mzazi atakuwa na fursa ya kuongea na kijana wake ili kujikinga na VVU, tumeendelea kutoa elimu mbalimbali ikiwamo ya kujipima kwa vijana walio na umri wa kuanzia miaka 18 na elimu kuhusu homa ya ini kwa vijana," alisema.

Mratibu huyo alibainisha malengo hayo ya serikali yametokana na kuona maambukizi ya VVU ni makubwa hasa kwa kundi la vijana, hasa vijana wa kike wenye umri wa kati miaka 15 hadi 24 ambao asilimia mbili wameambukizwa VVU kwa mujibu wa utafiti wa 2016 hadi 2017.

Alisema jitihada mbalimbali zimeendelea kufanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau wengine kwenye masuala ya VVU/Ukimwi kwa kuwa mkakati wa Wizara ya Afya ni kuhakikisha maambukizi yanapungua kwa asilimia 95 ifikapo mwaka 2030.

Akataka changamoto nyingine ya vijana ni kushindwa kufuata matumizi sahihi ya dawa ya kupunguza makali ya VVU, akihimiza wazazi na walezi kuwasimamia kuepusha usugu wa dawa.

Mkurugenzi wa Mtandao wa Kitaifa wa Wanawake Wanaoishi na VVU (NNW+), Veronica Lyimo alisema mwitikio kwa vijana kupima VVU ni mdogo kutokana na kuchelewa kupata elimu ya kutosha na kwa wakati.

"Kijana anatakiwa kuwa na uelewa juu ya mabadiliko ya mwili ili kumweka salama na kuepuka kupata maambukizi ya VVU akiwa katika umri mdogo.

"Pia anatakiwa kuepuka kushiriki ngono na kuwa kwenye hatari ya kupatwa na magonjwa mengine ambukizi," alisema.

Kuhusu wanawake kuwa mstari wa mbele kujitokeza kupima VVU kulinganishwa na wanaume, Veronica alisema kunatokana na wanaume kuwa na majukumu mengi, lakini mtandao hautachoka kufanya uhamasishaji kwa kundi hilo liwajibike kukabili maambukizo mapya ya VVU na afua zingine.



# Canada yavutiwa vita unyanyasaji kijinsia Tanzania

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KANSELA wa Ushirikiano na Maendeleo wa Ubalozi wa Canada, nchini Tanzania, Hellen Fytch, amesema serikali ya nchi hiyo inavutiwa na idadi ya wadau hai walioko kwenye vita dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia, huku kukiwa na taswira ya siku zijazo kwamba wanawake na watoto, wanaweza kufurahia haki yao ya kuishi bila unyanyasaji.

Alisema katika kuelekea mabadiliko ya kweli ya kisera, Serikali ya Canada, inaona iko hatua kubwa imepigwa na mashirika yasiyo ya kiserikali na wawakilishi wa jamii Tanzania katika masuala ya usawa wa kijinsia na haki za binadamu.

Kansela Fytch, alikuwa akizungumza na wadau mbalimbali mwishoni mwa wiki Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, wakati wa hafla ya kuhitimisha mradi wa kukuza usawa na elimu ya haki za binadamu (AEHRE).

Mradi huo wa miaka mitano, ulikuwa ukitekelezwa na Shirika la TUSONGE CDO, kwa ushirikiano na mashirika wenza 34, chini ya ufadhili wa Kituo cha Kimataifa cha Elimu ya Haki za Binadamu (EQUITAS).

"Majadiliano yenu muhimu yamesababisha kuimarishwa kwa mpango wa kitaifa wa utekelezaji wa miradi ya kukomesha ukatili dhidi ya wanawake na watoto, ambao tunatarajia kuuhitimisha hivi karibuni.

"Si hivyo tu, lakini Serikali ya Manispaa ya Moshi, iliazimia kutenga bajeti inayohusu masuala ya haki za wanawake. Hizi ni hatua kubwa kuelekea mabadiliko ya kweli ya sera, ambayo mmeongoza. Mnapaswa kujivunia mafanikio haya. Nina imani kwamba EQUITAS na TUSONGE CDO mtafanikiwa hata zaidi."

Katika kutaniko hilo, mashirika 35 yaliyoshiriki kwenye mradi huo kutoka Mkoa wa Arusha yalishiriki 17 na Kilimanjaro 18. Walikuwamo pia, wanajamii walioshiriki kwenye kazi za jamii, watu 120.

Awali, Mkurugenzi wa Shirika la TUSONGE CDO, Aginatha Rutazaa, alisema wakati mradi huo unahitimishwa, umeongeza chachu kubwa kwenye jamii, hasa ukilenga kutokomeza ukatili wa kingono dhidi ya wanawake, wasichana na watoto katika Manispaa ya Moshi, Siha (Kilimanjaro), Arusha Jiji na Meru (Arusha).

"Hitaji hili lilitokana na uhalisia wa stadi ya awali iliyofanyika kabla ya utekelezaji kuanza.

Lengo la mradi huu ilikuwa ni kuongeza uwezo wa wanawake na wasichana kukuza usawa wa jinsia ndani ya jamii zao kwa kutumia elimu ya haki za binadamu.

Aidha, kiongozi wa mila kutoka Mkoa wa Arusha, Furanael Nnko, akitoa ushuhuda kuhusu mafanikio ya elimu waliyoipata, alisema miongoni mwa waliyojifunza na kuona matokeo yake ni namna kuondoa visasili na mitizamo hasi ya ukatili wa kingono, ambayo ni muhimu katika kushughulikia visa hivyo.

# Wazee kimila wafugaji wakutana kujadili mgogoro ulishaji mifugo

**Na Mwandishi Wetu,** LONGIDO

ATHARI za mabadiliko ya tabianchi na usimamizi wa nyanda za malisho katika Wilaya ya Longido, mkoani Arusha, umewakutanisha pamoja viongozi wa mila wa jamii ya kifugaji ya Kimasai na serikali, kwa ajili ya kujadili utatuzi wa migogoro na hasara inayotokana na changamoto hizo.

Mkutano huo, ulioitishwa na Shirika la Watu na Wanyamapori Tanzania (TPW), linalotekeleza mradi wa ardhi kwa maisha, uliongozwa na Ofisa Mazingira kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Theodori Mlokosi.

Mkurugenzi wa TPW, Neovitus Sianga, alisema majadiliano hayo yanahusu njia bora za kusimamia nyanda za malisho na kushughulikia changamoto zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi.

Sianga, alisema kikao hicho pia kilijadili pamoja na mambo mengine, uwekaji wa mikakati madhubuti itakayowezesha jamii za eneo hilo, kuepukana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Kikao kilijikita pia kujadili maandalizi ya mipango ya msimu ujao wa malisho, ikizingatia mwanzo wa mvua katika eneo hilo.

...Tunataka kuanzisha mikakati ya kuimarisha usimamizi wa malisho, kwa kuzingatia hali ya hewa na rasilimali zinazopatikana kwenye maeneo haya," alisema Sianga.

Mmoja wa viongozi wa mila, Saroni Kayogo, alisema wako tayari kutoa mchango wao wa kiasili na utamaduni.

"Sisi viongozi wa mila wa jamii ya kifugaji ya Kimasai, tunalishukuru sana Shirika la TPW, kwa elimu na mafunzo waliotupa ya usimamizi wa nyanda za malisho na namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa ajili ya kuokoa mifugo kipindi cha kiangazi," alisema Kayogo.

Ofisa wa Mazingira wa TAMISEMI, Theodori Mlokosi, alisema matokeo ya kikao hicho ni hatua kubwa kuelekea kujenga ushirikiano imara, kati ya serikali, mashirika ya kiraia na jamii za asili.

"Kwa ujumla, kikao hicho kilimalizika kwa matumaini makubwa kwa mustakabali wa usimamizi wa malisho na mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi katika eneo la Longido na maeneo mengine yanayofanana nchini Tanzania.

"Kila mshiriki aliondoka akiwa na azma imara ya kuchukua hatua na kutekeleza mikakati iliyokubaliwa ili kuhakikisha uhifadhi wa mazingira na ustawi wa jamii."


**Air Tanzania**
The Wings of Kilimanjaro

## VACANCY ANNOUNCEMENT

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is expanding its network to meet the needs of its Business Strategy which focus on sustaining the recorded achievements and remain an airline of choice that meets and exceeds customers' expectations in line of its mission of provision of reliable, safe and high-quality services. Therefore, applications are invited from qualified Tanzanian to fill the position mentioned below:

**1. POSITION: SAFETY OFFICER II (1 POST)**

**1.1 QUALIFICATIONS**

- Must be holder of any Bachelor degree preferably Bachelor Degree in Science or ATPL or Flight Operations License or equivalent qualifications from recognized Institutions.
- Must have Certificate in Accident Investigation and Prevention or equivalent professional qualification
- Training in Quality Management System and/or safety management systems from a reputable organization shall be added advantage.

**1.2 RESPONSIBILITIES:**

i. Monitor status of Company Safety and emergency equipment's under supervision.
ii. Assist in monitoring through safety audit status of airports network.
iii. Carry out regular inspections of Company premises to identify issues that affect ground and flight safety.
iv. Prepare annual quality assurance program that provides for the auditing of the management system of operations, and maintenance functions.
v. Ensure equipment and operational products that are purchased or otherwise acquired from an external vendor or supplier meet the product technical requirements specified by the company prior to being used in the conduct of operations or aircraft maintenance.
vi. Ensure conformity with ICAO requirements by coordinating initial and renewal audits to air operators that transport company passengers under a commercial aviation agreement.
vii. Make follow up on findings that result from audits conducted under the quality assurance program by ensuring identification of root cause, development of corrective action appropriate to address findings, implementation of corrective action in appropriate operational area(s) and evaluation of corrective action to determine effectiveness.
viii. Prepare and coordinate the communication and coordination with operational managers in the management of operational risk.
ix. Prepare audit plan with sufficient resources and scheduled audits at intervals that meet regulatory and management system requirements including ensuring that are conducted within the scheduled interval.
x. Prepare and Maintain an electronic database for audits conducted under the quality assurance program
xi. Perform any other official duty as may be assigned by your supervisor.

**2. TERMS AND CONDITIONS:**

Ten (10) years contract with attractive remuneration and Fringe Benefits as per ATCL Salary Structure and Incentive Scheme.

**3. MODE OF APPLICATION:**

Interested applicants must submit a dully signed letter for consideration of the applications attached with the following:

i. A detailed curriculum vitae (CV);
ii. Certified copies of all certificates (including Secondary School and birth certificate), and other relevant certificates and licenses. (Applicants who have studied outside Tanzania should have their certificates approved by relevant authorities i.e Tanzania Commission for Universities (TCU) or National Examination Council- NECTA))
iii. Two recent passport size photographs;
iv. Names and addresses of at least two reputable referees;
v. Applicant's reliable contact address, email address and telephone numbers.

***Note: Misrepresentation of facts and qualifications during application shall warrant legal consequences. Previous applicants may re-apply.***

**4. CLOSING DATES:**

Applicants should reach the undersigned within 14 days from the first date of this announcement: -

**MANAGING DIRECTOR & CHIEF EXECUTIVE OFFICER**
**AIR TANZANIA COMPANY LIMITED,**
**P.O. BOX 543,**
**DAR ES SALAAM**







Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Kanali Michael Mntenjele (katikati) akisikiliza maelezo ya huduma za afya katika mojawapo ya mabanda kwenye maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika ngazi ya wilaya kwenye viwanja vya Nyamwaga wilayani humo kwa ufadhili wa Barrick North Mara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ndoa za utotoni zinavyoibua upya janga la fistula

**Na Waandishi Wetu**

NDOA za utotoni zimetajwa kuwa chanzo cha ugonjwa wa fistula kuendelea kuwa tishio katika maeneo mbalimbali ya Kanda ya Ziwa huku asilimia kubwa ya wagonjwa wanaopokewa hospitalini kwa tatizo hilo wakitajwa kuwa wasichana wenye umri wa miaka 17 hadi 20.

Tatizo hilo linaelezwa kuchangia asilimia nane ya vifo vitokanavyo na uzazi, asilimia 90 ya visa vya kujifungua watoto wafu huku wanawake 3,000 wakitajwa kupata tatizo hilo kwa mwaka na watoto wa kike waliopo kwenye ndoa za utotoni wakiwa hatarini zaidi kupata ugonjwa huo.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake na Afya ya Uzazi na Mratibu wa Huduma ya fistula wa Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando, Dk. Elieza Chibwe, aliiambia Nipashe kuwa fistula ya uzazi ni tatizo linalotokana na tundu ambalo halitakiwi kuwapo, linalotokea kati ya kibofu cha mkojo na uke pia njia ya haja kubwa.

Amesema tundu hilo husababisha mgonjwa kutokwa na haja ndogo au kubwa mfululizo kutokana na kushindwa kujizuia na hali hiyo inatokea kwa asilimia 85 ya wagonjwa wote wa fistula ambao wanatokwa haja ndogo muda wote kwa sababu wanashindwa kuzuia.

"Sababu ya ugonjwa huu ni uchungu pingamizi wa zaidi ya saa 48 mpaka 72 kabla ya mjamzito kujifungua ambapo hii husababishwa na mambo tofauti ikiwamo kubeba mimba katika umri mdogo, tamaduni, umbali mrefu kutoka sehemu alipo hadi kwenye huduma za afya na kuchelewa kupata huduma," alisema Dk. Chibwa.

Vilevile katika hospitali hiyo kwa mwezi wanapokea wagonjwa zaidi ya 20 wa fistula na kila wiki wanawafanyia upasuaji wagonjwa wanane ikiwamo wasichana wenye umri chini ya miaka 18 waliopata ugonjwa huo kutokana na kubeba mimba katika umri mdogo.

"Wagonjwa wengi wa fistula ni wasichana wenye umri chini ya miaka 20, sababu nyingi za kupata ugonjwa huo kwanza ni ya kibaiolojia, maumbile yao yanakuwa bado hayajakomaa kwa hiyo kumpata binti mjamzito mwenye umri wa miaka 15, 16 na 17, uwezo wake wa kujifungua ni mdogo kwa sababu nyonga zake zinakuwa bado hazijakomaa watoto hao wa kike wakipata uchungu pingamizi bila msaada asilimia kubwa wanapata fistula," alisema Dk.Chibwa

Alitaja ukubwa wa kichwa cha mtoto unakuwa hakuna uwiano na maumbile ya mzazi huku akitaja watu wenye umri kuanzia miaka 25 kuwa na uwezo mkubwa wa kujifungua mtoto mwenye kilo tatu salama kuliko mwenye umri wa miaka 17 kutokana na tofauti za ukomavu wa viongo vyao.

Njia za kukabiliana na ugonjwa huo ni kupambana na kudhibiti kwanza ndoa za utotoni, wajawazito wahudhurie kliniki kwa kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kutopata ugonjwa huo na ikitokea mtu kaupata atahudumiwa kwa wakati.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufani Bugando, Dk. Fabian Masaga, amesema jamii bado haina uelewa wa fistula na kutaka kuendeleza mapambano ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwaajili ya kudhibiti ugonjwa huo hali inayoenda sambamba na uelimishwaji wa wauguzi na wakunga kuhakikisha wanatoa huduma bora ya uzazi kwa wanawake.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Americares Foundation Tanzania, Nguke Mwakatundu, kila mwaka wanawake 2,500 hadi 3,000 wanapata ugonjwa wa fistula nchini huku kati yao 1,500 hadi 2,000 pekee wanaopatiwa matibabu ya ugonjwa huo na zaidi ya wagonjwa 1,000 wakikosa matibabu na kuufanya kuendelea kuwa tishio katika jamii.

Mratibu wa Elimu ya Afya kwa Umma na Masuala ya Fistula ya Uzazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, Rachel Ntongwisangu, alitaja imani za kishirikina pamoja na mila na desturi kuwa kikwazo katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

"Wapo wanaosema ugonjwa huu unasababishwa na kulogwa, laana au kufanya mapenzi na wanaume wengi wakati wa ujauzito na kusema mtazamo ambayo siyo sahihi," alisema Ntongwisangu.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa, Dk. David Mndeba, alisema katika kukabiliana na ugonjwa huo serikali imeendelea kutoa elimu kwa wananchi katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kudhibiti ndoa za utotoni, kuhudhuria kliniki wakati wa ujauzito pamoja na kujifungulia hospitalini na kwenye vituo vya afya.

Baadhi ya waathirika wa fistula kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa akiwamo Pendo Bonephas, mkazi wa Mara alisema alipata ugonjwa huo kutokana na kujifungua kwa njia ya upasuaji hivyo kukataliwa na mume wake ambaye pia aliitelekeza familia.

Mariam Lukas (18), mkazi wa Nyamagana aliiambia Nipashe kuwa alipata ujauzito katika kipindi cha miezi mitatu ya ndoa yake aliyoifunga akiwa na miaka 17 baada ya kushindwa kuendelea na masomo yake, alitaja kupatwa uchungu siku nzima kuanzia saa moja asubuhi hadi jioni.

"Ilipofika saa tano usiku nikaanza kusukuma, lakini mtoto akawa hatoki, wakanipeleka chumba cha upasuaji na kufanyiwa upasuaji, wahudumu wa afya walifanikiwa kuokoa maisha yangu, lakini mtoto alifariki, nilikaa hospitalini kwa wiki tatu baada ya hapo nikatolewa mpira wa kupitisha haja ndogo, lakini ilianza kutoka mfululizo na hicho ndicho chanzo cha mimi kuwa na tatizo hili," alisema Mariam.

# Madiwani waridhia mapendekezo bajeti ya CSR bil.2/-

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

BARAZA la Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama limeridhia na kupitisha mapendekezo ya Mpango wa Uwajibikaji wa Kampuni kwa jamii (CSR) kwa mwaka 2024 unaogharimu Shilingi bilioni mbili katika kuboresha sekta ya afya na elimu.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Khamis Katimba, alisema maagizo ya serikali yaliyotolewa katika kikao chao na Waziri wa Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa ni kuwa halmashauri zote nchini zinapaswa kutumia ukusanyaji mapato 'TAUSI' kudhibiti upotevu wa fedha.

Alisema halmashauri ina uhitaji wa madawati 8,712 viti na meza 4,902 huku akiwataka wajumbe wa baraza hilo kupendekeza miradi yenye tija katika jamii zao kupitia mpango CSR na yupo tayari kuhakikisha upungufu wa madawati na meza unapatiwa suluhisho.

Alitaja maeneo ya kipaumbele yaliyotolewa na uongozi wa Barrick Gold Mine kuwa ni afya pamoja na elimu na vipaumbele hivyo ni muhimu kutokana na kuwa msaada mkubwa kwa jamii katika kutekeleza majukumu yao ya kiuchumi.

Akiwasilisha mpango na bajeti ya CSR, Ofisa Mipango na Uratibu, Elkana Zabron, alisema kwa mwaka 2023 fedha za CSR, halmashauri ilipanga kutumia Sh. bilioni 1.9 katika sekta za afya na elimu na imeshatumia Sh. bilioni 1.35.

Kwa mwaka 2024 alisema halmashauri inatarajia kutumia Shilingi bilioni mbili kutoka katika chanzo hicho kinacholipwa na Mgodi wa Barrick na tayari halmashauri ikishirikiana na wataalamu kutoka Barrick-Bulyanhulu wamewezesha uibuaji wa vipaumbele.

Naye Mbunge wa Jimbo la Msalala, Alhaj Idd Kassim, aliitaka halmashauri kuhakikisha mpango uliowasilishwa unatekelezwa kwa vitendo na kwa wakati

kwa kuwa fedha inayotolewa na Barrick-Bulyanhulu si hisani bali ni takwa la kisheria.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Mibako Mabubu, alimhakikishia Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, kuwa maagizo na maelekezo yote yaliyotolewa na serikali yatatimizwa kwa wakati kwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji (W) na timu yake ya wataalam ni wasikivu.

Nipashe
Spotika



SABABU 5 LIVERPOOL KUWA NA WASIWASI MSIMU HUU UK. 12-13



RONALDO

# REKODI 5 ZA RONALDO AMBAZO MESSI SASA HATAWEZA KUZIVUNJA

**RIYADH,** Saudi Arabia

USHINDANI wa Cristiano Ronaldo na Lionel Messi ulitawala ulimwengu wa kandanda kwa zaidi ya muongo mmoja. Mastaa hao wawili sasa wanaelekea mwisho wa maisha yao bora zaidi ya uchezaji na wataingia katika historia kama wanasoka wawili bora zaidi wa wakati wote kuwahi kutokea.

Katika kilele cha nguvu zao, Ronaldo na Messi walisukumana kwa viwango visivyo na kifani walipokuwa wakichezea klabu mbili kubwa za soka nchini Hispania, Real Madrid na Barcelona.

Uzuri wao binafsi uling'ara huku wawili hao wakipigania kila taji lililokuwa kwenye mstari na kuvunja rekodi nyingi kwa kushindana.

Hapa tunaangalia rekodi tano za Ronaldo ambazo ni vigumu kwa Messi kuzivunja.

**#5 Idadi ya mechi za kimataifa**

Ronaldo kwa sasa anashikilia rekodi ya kucheza mechi nyingi za kimataifa kwenye mchezo huo. Mshindi huyo mara tano wa tuzo ya Ballon d'Or ameichezea Ureno jumla ya mechi 201 katika maisha yake ya soka.

Wakati huohuo, Lionel Messi anashika nafasi ya nane kwenye orodha hiyo akiwa ameichezea Argentina mara 177.

Ronaldo ana umri wa miaka miwili zaidi ya Messi na kuna uwezekano wa kutundika daluga zake mapema kuliko nyota huyo wa Argentina. Hata hivyo, anaimarika kwa sasa na Messi kufikia rekodi hiyo ni ngumu kwa sasa.

**#4 Kufunga mabao 50+ katika misimu sita mfululizo**

Ronaldo anachukuliwa kuwa mfungaji bora zaidi kuwahi kupamba mchezo huo. Uwezo wake wa kufunga mabao ulikuwa muhimu kwa mafanikio ya Real Madrid katika muongo mmoja uliopita. Fowadi huyo mashuhuri alikuwa mfungaji mahiri sana wakati alipokuwa Real Madrid.

Alifunga zaidi ya mabao 50 katika michuano yote kwenye misimu sita mfululizo kuanzia msimu wa 2010-11 hadi 2015-16 akiwa na Real Madrid. Ronaldo ana uwezekano wa kushikilia rekodi hiyo kwa muda mrefu sana kwa kuwa sasa Messi amechelewa kufikia mafanikio haya ya ajabu.

**#3 Asisti nyingi zaidi Ligi ya mabingwa Ulaya**

Uchezaji wa Ronaldo ni wa kufurahisha sana katika mchezo wake. Kutokana na ukweli kwamba alibadilika na kuwa mshambuliaji wa kati katika hatua za mwisho za kazi yake.

Ronaldo ametoa pasi za mabao 42 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Yeye ndiye mwenye asisti nyingi zaidi wa wakati wote katika historia ya mashindano hayo ya Ulaya kwa ngazi ya klabu. Messi yuko karibu kidogo kwani ametoa pasi 40 za mabao.

Hata hivyo, kutokana na wachezaji wote wawili kuondoka Ulaya, huenda namba hizi zikabaki kama zilivyo.

**#2 Mabao mengi timu ya taifa**

Ronaldo kwa sasa ndiye kinara wa mabao katika soka la kimataifa la wanaume. Amekuwa mchezaji wa kipekee kwa Ureno kwenye safu ya kimataifa na amekuwa tegemeo lao kuu la mabao kwa takriban muongo mmoja na nusu sasa.

Ameifungia Ureno mabao 123 katika maisha yake ya kimataifa. Aliipiku rekodi ya mchezaji wa zamani wa Irani, Ali Daei ambaye alikuwa na mabao 109 alipofunga mabao mawili kwa Ureno dhidi ya Jamhuri ya Ireland katika mechi ya kufuzu kwa Kombe la Dunia la FIFA mnamo Septemba 2021.

Messi ndiye mfungaji bora wa tatu katika soka la kimataifa la wanaume. Ametikisa nyavu mara 104 katika mechi 176 akiwa na Argentina. Huku Ronaldo akiendelea kuwa mshambuliaji mkuu wa Ureno licha ya kufikisha umri wa miaka 38, huenda akaongeza mabao zaidi kwenye mkusanyiko wake. Hilo linafanya hii kuwa rekodi isiyowezekana kwa Messi kuivunja.

**#1 Mabao mengi Ligi ya Mabingwa Ulaya**

Kwa sasa si Ronaldo wala Messi wenye uwezekano wa kucheza tena soka la Ligi ya Mabingwa Ulaya katika maisha yao ya soka. Ronaldo kwa sasa anaichezea Klabu ya Al-Nassr inayoshiriki Ligi Kuu ya Saudi Arabia na Messi anaitumikia Klabu ya Ligi Kuu Marekani (MLS, Inter Miami.

Katika hatua hii ya maisha yao ya soka, kurejea Ulaya na kuvuka makali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya inaonekana haiwezekani. Kwa hiyo, idadi yao katika shindano hilo inaweza kubaki bila kubadilika.

Ronaldo ndiye mfungaji bora wa muda wote katika Ligi ya Mabingwa. Gwiji huyo wa zamani wa Real Madrid na Manchester United amefunga mabao 140 katika michuano hiyo ya Ulaya. Messi anashika nafasi ya pili akiwa na mabao 129.

## ISIKUPITE

KWA mujibu wa ChatGPT, hawa ndio magolikipa 10 bora wa wakati wote; 10. Sepp Maier (Mjerumani), 9. Edwin Van der Sar (Mholanzi), 8. Iker Casillas (Mhispania), 7. Manuel Neuer (Mjerumani), 6. Peter Schmeichel (Mdenmark), 5. Oliver Kahn (Mjerumani), 4. Gianluigi Buffon (Mtaliano), 3. Gordon Banks (Muingereza), 2. Dino Zoff (Mtaliano), 1. Lev Yashin (Mrusi).



## Extra Time

# WACHEZAJI WATANO 'VIBABU' ZAIDI EPL



THIAGO SILVA

**LONDON,** England

KATIKA miaka ya hivi karibuni, wachezaji wa soka wamekuwa wakifurahia maisha marefu katika taaluma zao, ushuhuda ni kutokana na maendeleo katika sayansi ya michezo, kanuni za mazoezi ya mwili na ustawi wa jumla wa wachezaji.

**Hata hivyo, hali hii inakumbana na changamoto kubwa katika Ligi Kuu England (EPL), ambayo inajulikana kwa mahitaji ya nguvu ya kimwili.**

Ratiba ya kuchosha na ushindani mkali, huweka mkazo mkubwa kwenye miili ya wachezaji, na kufanya iwe vigumu kudumisha uchezaji wa kilele kwa muda mrefu.

Hali ya kasi ya juu ya Ligi Kuu England mara nyingi husababisha kuumia kwa wachezaji ikilinganishwa na ligi zingine. Hii, kwa upande wake, inahitaji usimamizi wa uangalifu wa mafunzo na vipindi vya kupona.

Kwa hiyo, kucheza hadi mwisho wa miaka 30 katika mazingira ya juu kwenye Ligi Kuu England ni mafanikio ya kupongezwa.

Sasa hapa tunawaangalia wachezaji watano wenyewe umri mkubwa zaidi kwenye Ligi Kuu England kwa hivi sasa (2023)...

### #5 Jonny Evans (Manchester United) - miaka 35

Jonny Evans alipanda ngazi katika Klabu ya Manchester United na hatimaye kuwa nyota wa kikosi cha kwanza msimu wa 2007-08. Alishinda mataji matatu ya Ligi Kuu, taji moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya, mataji mawili ya Kombe la Klabu Bingwa Dunia katika kipindi chake cha kwanza katika klabu hiyo.

Evans alizichezea West Bromwich Albion na Leicester City na alikuwa na sifa kama beki wa kati wa kutegemewa kwenye Ligi Kuu. Baada ya kuachiwa kutoka Leicester mwishoni mwa msimu wa 2022-23, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, alianza mazoezi na Manchester United.

Baadaye alisaini mkataba wa muda mfupi na United na hilo sasa limekuwa na manufaa baada ya mabeki kadhaa wa United kupata majeraha.

### #4 Tim Ream (Fulham) - miaka 36

Mchezaji wa Kimataifa wa Marekani, Tim Ream, aliingia uwanjani kwenye Ligi Kuu ya soka ya Marekani (MLS), akichezea New York Red Bulls kati ya mwaka 2010 na 2011, ambapo alionesha umahiri wake kwenye ulinzi. Kisha alijiunga na Bolton Wanderers mwaka 2012 na kushinda tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwaka mara mbili katika muda wake wa miaka mitatu katika klabu hiyo.

Ream baadaye alihamia Fulham mnamo Agosti 2015 na anaendelea kuwa kwenye klabu hiyo hadi leo. Kwa sasa akiwa na umri wa miaka 36.

### #3 James Milner (Brighton & Hove Albion) - miaka 37

James Milner asiyechoka sasa yuko katika tafrija ya kazi yake. Amefurahia maisha mazuri na amejitokeza kwa baadhi ya timu kubwa nchini England zikiwamo Manchester City, Liverpool, Newcastle United, Aston Villa, Leeds United na Brighton & Hove Albion.

Milner anasifika kwa maadili yake ya kipekee ya kazi na utengamano uwanjani, akibadilika katika nyadhifa mbalimbali kwa kujitolea bila kuyumbayumba.

Akili yake, ujuzi wa kimbinu na sifa za uongozi zilimfanya kuwa mchezaji muhimu kwa Manchester City na Liverpool. Amechangia si tu kupitia uchezaji wake thabiti, lakini pia kwa kuweka kiwango cha juu cha taaluma na kujitolea ndani ya kikosi.

Milner kwa sasa anaichezea Brighton na ni mmoja wa wachezaji wakongwe kwenye Ligi Kuu England.

### #2 Ashley Young (Everton) - miaka 38

Ashley Young bado anaendelea vema akiwa na umri wa miaka 38. Mwingereza huyo mwenye kipaji cha kiufundi, amezichezea klabu kadhaa na kufanya vema katika nafasi kadhaa. Katika kipindi cha kazi yake adhimu, Young ameonesha uwezo wa kukabiliana na mahitaji ya hali hiyo na kujiboresha zaidi.

Amezichezea Watford, Aston Villa, Manchester United, Inter Milan na Everton katika maisha yake ya soka ambayo sasa yamedumu kwa zaidi ya miaka 20.

Muda mzuri wa Young bila shaka ulikuja akiwa na Manchester United, ambapo alishinda taji moja la Ligi Kuu, moja la Kombe la FA, Kombe la Ligi moja na taji moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 38, pia alishinda taji la Serie A akiwa na Inter Milan msimu wa 2020-21.

### #1 Thiago Silva (Chelsea) - miaka 39

Thiago Silva ni mmoja wa mabeki bora wa kati kwenye Ligi Kuu England hivi sasa. Inashangaza kwamba anaendelea kuwa wa kiwango cha kimataifa licha ya kufikisha miaka 39 mnamo Septemba mwaka huu. Silva anazingatiwa sana kama mmoja wa walinzi wakubwa wa kizazi chake na amekuwa akitoa kiwango cha juu kwa klabu na nchi.

Amechezea klabu kama Dynamo Moscow, Fluminense, AC Milan, Paris Saint-Germain na Chelsea. Maisha ya Silva yanachukua zaidi ya miongo miwili na pia amekuwa sehemu ya Timu ya Taifa ya Brazil tangu 2008, na kuwachezea Selecao hao mara 113.

Silva ameshinda mataji saba ya Ligue 1, taji moja la Serie A, taji moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya, moja la Copa America, moja la Shirikisho la FIFA, moja la kalbi bingwa ya Dunia, mataji matano ya Coupe de France na sita ya Coupe de la Ligue katika maisha yake ya soka.

## Nukuu

"Sifikirii kuhusu Kombe la Dunia na siwezi kusema kwamba sitakuwapo pia kwa sababu kila kitu kinaweza kutokea baadaye. Kutokana na umri na hali itakavyokuwa, jambo la kawaida zaidi ni kwamba sitakuwapo, lakini tutaona nini kitatokea, siwezi kusema sasa," **Lionel Messi alipoulizwa endapo atakuwapo kwenye Kombe la Dunia lijalo.**



"Sikuwa na mshangao wowote au shaka yoyote (kuhusu uwezo wa Jude Bellingham), lakini labda jambo moja la kushangaza ni jinsi alivyofanya hivi haraka. Nilicheza na Figo [Luis] na Zidane [Zinedine] na, hata kwao, ilichukua muda. Nakumbuka Zizou alipofika hapa, mwezi wa kwanza au miezi miwili, hakuwa mzuri kama alivyokuwa Juventus. Lakini kwa utu na tabia ya Jude, inaonekana amekuwa akicheza hapa Madrid kwa miaka kumi," **Mchezaji wa zamani wa Real Madrid, Aitor Karanka.**



"Pale Barcelona, hatukuruhusiwa kumgusa mazoezini. Hiyo inaonekana kuwa ni ya mbali lakini ni kweli, tulipaswa kuwa makini (kwa kutotomia nguvu dhidi yake), hiyo ni kawaida. Yeye ni GOAT! (Mchezaji Bora wa Wakati Wote) Hutataka kumjeruhi," **Beki wa zamani wa Barcelona, Jean-Clair Todibo, ambaye alicheza pamoja na Messi pale Nou Camp kwa miaka miwili, akielezea jinsi walivyotakiwa kumlinda kazini. Todibo kwa sasa anaichezea Nice ya Ufaransa.**





Straika wa Simba, Jean Baleke, akipasua katikati ya mabeki wa timu ya Jwaneng Galaxy, wakati timu hizo zilizo Kundi B, zilipochuana juzi kwenye Uwanja wa Obed Itani Chilume nchini Botswana na kutoka suluhu. **PICHA: SIMBA**

# MATUKIO, REKODI, TAKWIMU ZA SIMBA, YANGA LIGI YA MABINGWA

**Na Adam Fungamwango**

WAWAKILISHI wa Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi, Simba na Yanga, juzi walilazimishwa sare katika michezo yao za raundi ya pili na kuondoka na pointi moja katika mechi zilizochezwa Dar es Salaam na Francistown nchini Botswana.

**Wakati Simba iliyo Kundi B ikitoka sare bila kufungana na wenyeji wao, Jwaneng Galaxy kwenye Uwanja wa Obed Itani Chilume nchini Botswana mechi iliyochezwa mapema, saa 10 jioni, Yanga ililazimishwa sare ya bao 1-1 na Mabingwa Watetezi, Al Ahly ya Misri, mechi ikichezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, saa 1:00 usiku katika mchezo wa Kundi D.**

Ni matokeo ambayo yameziweka timu hizo kwenye mazingira magumu kidogo ingawa bado zina nafasi ya kusonga mbele kama zitafanya vema kwenye michezo minne ijayo kwa kila timu.

Kuna matukio yaliyojitokeza kwenye mechi zao za juzi, rekodi mbalimbali na takwimu, ambayo tunakuletea katika makala haya kwa mtindo wa namba, twende sasa...

**90 -** Wanachama na mashabiki wa Simba hawatoisahau dakika hiyo, kwani muda mfupi tu kabla ya mechi kumalizika, Clatous Chama alipiga shuti la mguu wa kushoto lilikwenda kugonga mlingoti wa pembeni kwa chini na kurudi uwanjani, ukamkuta Baleke ambaye alipiga shuti kubwa juu ya lango.

**89 -** Ni dakika ambayo Yanga ilisawazisha bao katika mechi ya juzi dhidi ya Al Ahly, likiwekwa ndani ya kimia na raia wa Ivory Coast, Pacome Zouzoua, akipokea pasi kutoka kwa Mzambia, Kennedy Musonda, mechi ikaisha kwa sare ya bao 1-1.

**87 -** Yanga iliruhusu bao kizembe kwenye dakika hii, wakati Karim Fouad alipopiga krosi, iliyosababisha mabeki na kipa wao kuchanganyana. Nahodha Bakari Mwamnyeto alipojaribu kuondoa mpira huo kwa kichwa, kumbe alikuwa akitoa pasi kwa Percy Tau aliyeutumbikiza kimyani kwa kichwa.

**73 -** Kipa wa Yanga, Djigui Diarra aliokoa mpira wa hatari akiwa anatazamana na Taher Mohamed, alipotoka kidogo kulibana lango, kabla ya kuupangua mpira kwa mikono yake miwili, huku benchi la ufundi la Al Ahly likiwa limeshasimama kutaka kushangilia goli.

**33 -** Ni dakika ambayo Yanga ilipata pigo baada ya beki wake wa kushoto, Joyce Lomalisa, kuumia na kushindwa kuendelea na mchezo, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi akalazimika kumuingiza Nickson Kibabage kuchukua nafasi yake.

**32 -** Hii ni dakika ambayo, Aziz Ki alikuwa karibu kuipatia Yanga bao alipounganisha krosi ya Lomalisa na kuonekana unaingia wavuni baada ya kumgonga kipa El Shenawy, kwa mshangao ukatoka nje sentimeta chache.

**24 -** Ni dakika ambayo Jeen Baleke alipata nafasi ya kubaki ana kwa ana na kipa, akiwa ana kwa ana na kipa Goitseone Phoko, lakini shuti lake liliishia mikononi mwa kipa huyo.

**9-** Ilikuwa ni dakika hii wakati kipa wa Simba, Ayoub Lakred, alipoiokoa timu yake isifungwe bao kutokana na shambulizi kali la kushtukiza, wakati straika wao hatari Daniel Msendami alipoupata mpira mrefu na kuanza kuwatoka mabeki wa Simba mmoja baada ya mwingine, kabla ya kutaka kuuweka wavuni, lakini Lakred aliruka na kutumia mguu kuokoa hatari hiyo.

**4 -** Ni idadi ya mabao ambayo Yanga imeruhusu kwenye michuano hiyo mpaka sasa, ikifungwa mabao 3-0 katika mechi ya kwanza dhidi ya CR Belouizdad ya Algeria, Novemba 24, pamoja na mechi ya juzi dhidi ya Al Ahly. Namba hii pia inasimama kwa nafasi inayoshika Yanga kwenye msimamo wa Kundi D, ikishika mkia na pointi moja iliyonayo mpaka sasa.

**3 -** Simba inashika nafasi hii kwenye msimamo wa Kundi B mpaka sasa na hii ni baada ya Asec Mimosas kuifunga Wydad Casablaca bao 1-0 juzi usiku nchini Ivory Coast.

**2 -** Simba imetoa sare mara mbili katika michezo miwili, nyumbani dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast na juzi ikiwa ugenini dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana, ikiwa pia na pointi mbili.

**1-** Namba hii inasimama kwa timu zote mbili, Simba na Yanga zikiwa zimefunga bao moja tu mpaka sasa, Saido Ntibazomkiza akifunga upande wa Wekundu wa Msimbazi katika mechi dhidi ya Asec Mimosas kwenye sare ya bao 1-1, na Pacome Zouzoua akipachika upande wa Wanajangwani katika mechi ya juzi. Pia namba hiyo inasimama kwa Yanga kuwa imepoteza mechi moja mpaka sasa kwenye Ligi ya Mabingwa hatua ya makundi.

**0 -** Timu zote mbili, hazijashinda mechi yoyote ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi mpaka sasa msimu huu, lakini Yanga ikiendeleza rekodi yake ya kutoshinda mchezo wowote wa hatua hiyo tangu mfumo huo wa makundi uanzishwe.

## JE, WAJUA?



HADI Ligi Kuu England inaingia mechi za raundi ya 14, Arsenal ikiwa kileleni, ndiyo timu iliyoruhusu mabao machache zaidi (11), idadi sawa na Liverpool, huku Manchester City ikiwa timu pekee iliyofunga mabao mengi zaidi kuliko zote (33), ikifuatiwa na Newcastle (32), wakati Sheffield ikiwa ndiyo timu iliyoruhusu mabao mengi zaidi (39), lakini pia ndiyo inayoburuza mkia wa ligi hiyo.



# Washauri Sheria Malipo Fidia ipitiwe upya

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MKALAMA

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, mkoani Singida, wameitaka serikali kuifanyia mabadiliko Sheria ya Malipo ya Fidia kwa wananchi ambao mazao yao yanaharibiwa na tembo mashambani kutokana na kiwango kinachotolewa kwa waathirika kuwa kidogo kulinganisha na athari wanazopata.

Diwani wa Kata ya Mwangeza, Bosco Samweli, akizungumza juzi kwenye kikao cha robo ya kwanza cha kujadili utekelezaji wa miradi, alisema maeneo mbalimbali katika Wilaya ya Mkalama, wananchi wanakumbwa na uvamizi wa tembo kwenye nyumba zao na uharibifu wa mazao mashambani.

Mwangeza, alisema kiwango cha Sh. 100,000 kinachotolewa kwa waathiriwa wa mashamba na Sh. 1,000,000 kinachotolewa kama kifuta jasho kwa wanaopoteza maisha ni kidogo na kuwapo haja ya kubadili sheria hiyo ili kiwango cha malipo ya fidia na kifuta jasho kiongezeke.

Diwani wa Kata ya Kikhonda, Elisha Kanka, alisema suala la upatikanaji wa Vitambulisho vya Taifa limekuwa kero kwa wananchi na kuitaka serikali isogeze huduma za karibu na wananchi.

Naye Diwani wa Kata ya Nkinto, Reuben Charles, alisema mbegu za alizeti za ruzuku zinazotolewa na serikali kwa mfululizo wa miaka miwili ya msimu wa kilimo hazistawi vizuri jambo linalowakatisha tamaa wananchi.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Abdalla Njelu, akijibu hoja ya tembo, alisema wilaya hiyo wananchi wanapata changamoto ya tembo na suala la kutaka kiwango cha malipo na fidia na kifuta jasho kiongezwe watali-wasilisha katika ngazi husika.

Katika hatua nyingine Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama mkoani Singida, imeadhimisha miaka 10 tangu kuanzishwa huku mafanikio lukuki yakielezwa yakiwamo kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato kutoka Sh. milioni 247 zilizikusanywa katika bajeti ya 2013/2014 hadi kufikia Sh.bilioni 1.749 ambazo zinazokusanywa hivi sasa.

Kaimu Afisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya Mkalama, Daniel Tesha, akielezea mafanikio hayo katika maadhimisho yaliyowashirikisha madiwani, watendaji wa vijiji na kata, wakuu wa idara na viongozi wa serikali, alisema mafanikio hayo yamepatikana kutokana na ushirikiano mzuri wa watumishi katika halmashauri hiyo.

Tesha alisema katika kipindi cha miaka 10, halmashauri hiyo imepata hati safi mfululizo miaka tisa na moja yenye mashaka. Wilaya ya Mkalama ilianzishwa Julai 2012 baada ya kumegwa kutoka Wilaya ya Iramba.



Naibu Katibu Mkuu wa Kanisa la Pentecoste Holliness Association Mission Tanzania (PHAM T) Julias Bundala,akiwalisha keki watoto wa Kituo cha Infinity Glory Daycare and Nursery School baada ya kuhitimu elimu ya awali kwenye sherehe ya mahafali yaliyofanyika jana wilayani Kongwa. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Aagiza upandaji miti, utunzaji mazingira endelevu

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Dk. Semistatus Mashimba, ameagiza wadau wa mazingira mpango wa upandaji miti na utunzaji wa mazingira unakuwa endelevu.

Dk. Mashimba aliyasema hayo juzi wakati wa upandaji miti katika Shule ya Msingi Mahama ulioandaliwa na Shirika lisilo la kiserikali la Equality for Growth.

Alisema ajenda ya utunzaji wa mazingira inatakiwa kuzingatiwa kila siku kuanzia ngazi ya mitaa, vijiji, kata, halmashauri na wadau wa mazingira linakuwa endelevu.

"Naomba nitoe maelekezo kwa wadau wa mazingira wote katika halmashauri yetu, naomba tuzingatie suala la upandaji miti, lakini sio tu kupanda bali na kuisimamia ikue, tusiwe tunapanda miti na kuiacha ife."

"Lakini pia msiishie katika shule tu za mijini, twende kwenye taasisi zetu zote shule, vituo vya afya na huko walioko pembezoni, kule nako tuwafikie maana kuna uharibifu mkubwa wa mazingira, viongozi wa vijiji, kata na maofisa, agenda ya utunzaji wa mazingira iwe kila siku," alisema Dk. Mashimba.

Aidha, ili mazingira yanabaki kuwa safi, shirika hilo limewawezesha mashine ya kuchakata mkaa mbadala kikundi cha kufanya usafi cha Mazengo Land's care kilichopo Chamwino Ikulu ili kutunza mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Mmoja wa wanakikundi hicho, Malisela Mamba, alisema mashine hiyo itawawezesha kiuchumi kwa kuinua kipato, na kuhakikisha mazingira yanabaki kuwa salama kwa kupata mkaa bila ya kukata miti.

"Kikundi chetu kinahusika na utunzaji wa miti na uoteshaji wa miti ya matunda, kivuli na maua, hadi sasa tuna miche 1,000 na lengo letu ni kufikia miti 5,000," alisema Mamba ambaye ni mhasibu wa kikundi.

# Wazazi na walezi watakiwa kuwa mabalozi kupinga ukatili

**Na Peter Mkwavila,**
KONGWA

NAIBU Katibu Mkuu wa Kanisa la Pentecoste Holliness Association Mission Tanzania (PHAM T), Askofu Julias Bundala, amewaomba wazazi na walezi wilayani Kongwa kuwa mabalozi wa kupiga vita viendo vya mmomonyoko wa maadili ambao umeshamiri katika jamii hususani kwa vijana na watoto.

Askofu Bundala, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na wazazi na walezi wilayani hapa, kwenye sherehe za maahafali ya kituo cha Infinity Glory Daycare and Nursery School yaliyofanyika mtaa wa Majengo.

Bundala, alisema maendeleo ya taifa yanategemea nguvu kazi na nidhamu watakayojengewa watoto, wajibu wa malezi na misingi ya kiroho yanategemea wazazi ambao ni mabalozi wakubwa kwa upande wa serikali na madhehebu ya dini.

"Wazazi na walezi mkaendelee kuwalea hao watoto ambao leo hii wameanza hatua nyingine ya kupata elimu zaidi na pia mkawe mabalozi wazuri katika kuhakikisha hawa watoto hawajiingizi kwenye vita hii ya mmomonyoko wa maadili," alisema.

Kadhalika, aliwasihi wazazi na walezi kuendelea kuliombea taifa amani, utulivu, upendo na mshikamano ili kulijenga taifa bora na lenye maendeleo duniani.

"Sina shaka na nyinyi wazazi na walezi pamoja na majukumu ya kuwalea watoto mtaendelea kuiombea nchi pamoja na viongozi waliopo ndani ya serikali na madhehebu ya dini waweze kudumu kwenye upendo na uaminifu," alisisitiza.

Mkurugenzi wa Kituo cha Infinity Glory Daycare and Nursery School, Geofrey Sakila, alisema ni imani kuwa watoto hao wanaenda kuanza hatua nyingine ya elimu ambayo itawasaidia kuwajengea misingi ya kiroho.

Aliwataka wazazi na walezi wa wilaya hiyo kuwaandikisha watoto wao kwenye vituo vya shule za awali ambavyo vimesajiliwa. Alisema hivi sasa kuna utitiri wa vituo vya watoto wadogo (Nursery School) vimeanzishwa lakini havina usajiri,na vipo kwa ajili ya kujipatia fedha badala ya kumwendeleza mtoto kitaaluma na kielimu zaidi.



# Wakulima waomba wachakachuaji mbolea waadhibiwe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKULIMA mkoani Njombe wameiomba serikali kuwadhibiti mawakala wa mbolea wasio waaminifu ambao wanachakachua mbolea na kusababisha hasara kubwa kwao.

Ombi hilo walilitoa kwenye mkutano wa wadau wa kilimo Nyanda za Juu Kusini, ulioandaliwa na kampuni ya mbolea ya INTRACOM, uliofanyika mkoani hapa.

Walisema mawakala wenye tabia za kuchakachua mbolea wanatakiwa kupewa adhabu kubwa ili kutoa fundisho kwa wengine wenye tabia hizo.

Baadhi ya wakulima hao, Frank Mwenda alisema, mawakala wa mbolea wanatakiwa kuepuka kuingia kwenye mkumbo wa kuuza mbolea iliyochakachuliwa kama ilivyofanywa na wenzao katika msimu wa kilimo uliopita na kusababisha kashfa kwa mkoa.

"Kwa hiyo serikali isimamie zaidi na watu wanaochakachua mbolea wapate adhabu kubwa ili kuwa mfano kwa wengine wasiweze kufanya hivyo," alisema Mwenda.

Mkuu wa Wilaya ya Makete, Juma Sweda, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alisema Mkoa wa Njombe, una mahitaji ya mbolea zaidi ya tani 112, lakini mpaka sasa lengo hilo halijafikiwa.

Alisema kuwapo kampuni ya mbolea kunatoa fursa kwa wakulima wa mkoa huo kuongeza tija na kipato kwenye maeneo hayo.

"Tunaipongeza sana Intracom kwa uamuzi wake muhimu na mzuri katika Nyanda za Juu Kusini kwani mbolea hii itaongeza tija na kipato kwa wakulima," alisema Sweda.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Mbolea ya Intracom, Nazaire Nduwimana, alisema kiwanda hicho kupitia mbolea ya Fomi kina mchango mkubwa katika mapinduzi ya kilimo nchini.

"Huwezi kuzungumza kilimo bila ya kutaja mbolea na mbolea inayohitajika ni ile iliyosahihi na inayoweza kumkomboa mkulima na kuinua kipato chake na kukuza uchumi," alisema Nduwimana.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Katibu Tawala Wilaya ya Mufindi, Frank Sichalwe, alisema nchi inakwenda kupiga hatua ya kutoka kutegemea mbolea zinazoagizwa kutoka nje na badala yake kuwa na mbolea ambayo inazalishwa nchini.

"Na malighafi zake ni samadi za wanyama, samadi za ndege kutoka kule Mkoa wa Manyara ndizo zinatumika kuzalisha...," alisema Sichalwe.

Meneja Mkuu wa Kampuni ya Mbolea ya Mtewele Traders imkoani Njombe, Sady Mwang'onda, alisema uchakachuaji wa mbolea mara nyingi hutokea bidhaa inapokuwa adimu uwapo wa mbolea ya Fomi unakuja kupunguza changamoto ya mbolea kwa wakulima na kuondoa kabisa uchakachuaji.

"Uchakachuaji wa mbolea mara nyingi hutokea pindi bidhaa inapokuwa adimu kwahiyo upatikanaji wa mbolea za kutosha unakwenda kuondoa uchakachuaji...," alisema Mwang'onda.

# TCRA yaanzisha kampeni 'Leseni Kidijitali'

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, imeanzisha kampeni maalumu ya kuhamasisha watoa huduma za mawasiliano kuhusu namna ya kuomba leseni kwa njia ya kidigitali itwayo 'Leseni Kidijitali' ambayo inalenga kurahisisha upatikanaji.

Kampeni hiyo imeambatana na utoaji wa elimu kuhusu namna ya kuboresha huduma za mawasiliano ili waaminiwe na wadau NA watumiaji wa huduma hizo.

Akizungumz na wandishi wa habari mwishoni mwa wiki, Meneja wa TCRA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mhandisi Asajile John, alisema lengo la kampeni hiyo ni kuongeza uelewa kwa watoa huduma wa sekta hiyo.

Alisema mamlaka hiyo inatoa elimu kwa wananchi kwa njia ya redio zilizoko katika kanda hiyo yenye mikoa ya Mbeya, Iringa, Rukwa, Ruvuma, Katavi, Njombe na Songwe.

Alizitaja leseni zinazotakiwa kuombwa kwa njia ya kidijitali kuwa za usafirishaji wa vipeto, leseni za maudhui ya habari za mtandaoni na za kuagiza na kusambaza vifaa vya mawasiliano ambazo zinapatikana kupitia mfumo maalumu wa 'Tanzanite portal'.

"Huhitaji tena kutembelea ofisi zetu ili kupata leseni, unaweza ukaomba ukiwa popote, tumefanya hivyo ili kuwarahisishia wateja wetu na mchakato huu umekuwa rahisi sana na yeyote anaweza akautumia mfumo huu," alisema Mhandisi Asajile.

Aliwataka watoa huduma za mawasiliano kuwa na leseni zinazowaruhusu kufanya kazi hiyo na kutoa huduma bila leseni ni kosa kwa mujibu wa sheria na wanaweza wakachukuliwa hatua.

Ofisa Mawasiliano wa TCRA, Robin Ulikaye, aliwasisitiza wananchi kuwatumia watoa huduma waliosajiliwa ili kulinda haki haki zao.

"Njia ya kuthibitisha uhalali wa leseni ya mtoa huduma uliyochagua ni rahisi sana ni kwa kutumia simu ya mkononi unaweza ukapiga *152*00# na ufuate taratibu za uhakiki kwa kuingiza nambari ya leseni ya mtoa huduma wako," alisema Ulikaye.

Ulikaye aliwahimiza watoa huduma za mawasiliano ambao wamesajiliwa, wakiwamo wanaojihusisha na habari za mtandaoni, wasafirishaji wa vifurushi, watangazaji, mafundi simu na wafungaji wa vifaa vya mawasiliano kutumia tovuti hiyo kuhuisha leseni zao.

Alisema TCRA haitoi leseni kwa wauzaji wa vifaa vya mawasiliano, lakini inawataka wahakikishe wanaponunua vifaa hivyo kwa ajili ya biashara zao za rejareja wanavinunua kutoka kwa waagizaji na wasambazaji wenye leseni.

TCRA imeanzisha kampeni hiyo ikiwa ni sehemu ya kusherehekea miaka 20 tangu ilipoazishwa mwaka 2003 na kuboresha huduma kwa njia mbalimbali kulingana na mabadiliko ya teknolojia.




Mkurugenzi Mkuu wa Vivo Energy Tanzania Mohamed Bougriba (kulia) akikabidhi moja kati ya vifaa kwa ajili ya wanafunzi wenye uhitaji maalumu wa Shule ya sekondari ya Jangwani kwa mwanafunzi, Sikujua Selestine, kampuni ya Vivo Energy ilikabidhi taulo za kike, viungo bandia na magongo kwa wanafunzi hao. Kushoto ni Makamu Mkuu wa shule hiyo, Paulina Aweda. Hafla hiyo ilifanyika mwishoni mwa wiki Jangwani jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanaume wasiotunza watoto kupewa adhabu ya kutoa bati 2

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MWENYEKITI wa Mtaa wa Kambarage Halmashauri ya Mji Njombe, Mkoa wa Njombe, Francis Msanga amesema wamejipanga kutokomeza udumavu kwa kuanzisha sheria ndogo ndogo kwa wanaume ambao hawatunzi watoto kwa kuwapa adhabu ya kutoa bati mbili.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na wananchi wa mtaa huo katika kuhitimisha kampeni ya lishe, kuwa hatua hizo lazima zichukuliwe ili kuwawajibisha wanaume hao ambao huwaachia jukumu la malezi wanawake peke yao.

"Tunatoa elimu kwanza watunze mtoto kuliko kitu chochote kwasababu kutafuta mtoto ni kazi ngumu kuna watu wanatafuta watoto hawapati kwahiyo tunawaambia watoto wawatunze," alisema Msanga.

"Mimi maagizo yangu kwa wanaume iwe msibani, iwe wapi, kwenye mtaa wangu nimewaambia wanawake wanapoona mwanaume ajishughulishi na chochote wamlete ofisini mimi nina shida ya kujenga ofisi, anapigwa bati mbili halafu baada ya hapo anaenda kufanya kazi ya kuleta huduma kwa watoto," alisema.

Ofisa Tarafa wa Njombe Mjini, Liliani Nyemele kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Njombe, alitoa rai kwa wazazi na walezi kutumia muda katika malezi ya watoto badala ya shughuli za kiuchumi.

"Nawaomba wazazi na walezi hakikisheni mnatumia muda mwingi kuhudumia familia ili watoto wenu waweze kupata lishe bora," alisema Nyemele.

Nyemele aliitaka jamii kuweka utamaduni wa kuhakikisha wanapanda matunda na mboga kwa wingi katika maeneo yao ili kuimarisha afya za watoto wao.

Ofisa Lishe Halmashauri ya Mji Njombe, Damiana Danda, alisema ni muda sasa kwa wazazi na walezi kusimama kidete kutokomeza udumavu mkoani humo katika kuzingatia matumizi bora ya vyakula makundi yote.



## KIST yapewa mbinu kuongeza kasi maendeleo teknolojia

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk Khalid Salum Mohamed, ameitaka Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknelojia (KIST), kuimarisha utafiti na kukuza ubunifu ili kuongeza kasi ya maendeleo ya teknolojia nchini.

Aliyasema hayo jana katika mahafali ya tisa ya Taasisi hiyo kwa wahitimu 522, wa fani mbalimbali, Mbweni Unguja.

Alisema hatua hiyo itasaidia kujielekeza zaidi katika ufundishaji na utafiti unaochangia na kurahisisha utekelezaji wa mipango ya nchi.

Aidha, alisema taasisi hiyo ni chachu ya kutoa wahitimu wanaohitajika katika maeneo yaliyopewa kipaumbele na serikali ya awamu ya nane, ambayo inafanya kazi kubwa kujenga mazingira ya uchumi na utoaji huduma bora za jamii.

Alisema, serikali imetenga eneo la hekta 71 kwa ajili ya masula ya Tehama na kuanzisha kituo cha IT Madrasa kwa lengo la kukuza ubunifu na teknelojia nchini.

Dk. Khalid aliupongeza uongozi wa taasisi ya KIST, kuona umuhimu wa kuongeza na kuanzisha kozi nyingine mpya ya stashahada, kwa uhandisi wa vifaa tiba, stashahada ya ualimu wa ufundi na shahada ya kwanza katika fani ya habari mawasiliano na teknelojia na ICT ya Multimedia.

Alisema kuwa fani ya uhandisi wa vifaa tiba itasaidia kuondoa tatizo la uhaba wa wataalamu katika mahospitali ambazo zimeimarishwa kwa vifaa tiba.

Aliwataka wanafunzi na wafanyakazi wa taasisi hiyo kufanya kazi kwa bidii, ushirikiano na maarifa ili kuleta mafanikio ya kuingia katika soko la ushindani wa ajira kwa sekta binafsi na serikali.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Khamis Abdallah Said, alisema wizara inaridhishwa na utendaji wa taasisi hiyo, ni vyema kuongeza bidii ili kupata wataalamu wa kutosha wa eneo la anga na kujenga uchumi wa nchi.

Mwenyekiti wa Baraza la Taasisi ya KIST, Dk. Afua Khalfan Mohammed, alipongeza serikali kuweka mazingira mazuri kwenye sekta ya elimu kwenye maeneo mbali mbali, pia taasisi hiyo imepiga hatua kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknelojia duniani ili kutoa wataalamu bora.

Mkuu wa KIST, Mahmoud Abdulwahab Alawi, alisema wamefanikiwa kuongeza fani mbili mpya za Sayansi, kupiga hatua kutoka wanafunzi 1512 kwa mwaka 2022 -2023 hadi wanafunzi 1927 kwa mwaka wa masomo 2023 -2024.

Alisema wahitimu 522 kati yao 328 Astashahada, 179 Stashahada na 15 ni Shahada ya kwanza ambao ni mafunzo ya matengenezo ya ndege.

Aliiomba Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuweka mazingira ya kujifunza kwa vitendo kupitia wizara hiyo, ili kuongeza weledi, ukuaji uchumi na ajira kwa wanafunzi kabla na baada ya kamaliza masomo.

Akisoma risala katika mahafali hiyo, Kauthar Ibrahim Makame, alisema taasisi ya KIST, imefanikiwa kutanua maabara ya sayansi kujenga ghorofa moja, dahalia la wanawake.

Alitaja baadhi ya changamoto za taasisi hiyo ni, ukosefu wa walimu wa kudumu, ugumu wa vitendea kazi, barabara inayoelekea kwenye eneo la anga na ukumbi mkubwa wa mitihani.

# Makamu ataka utafiti talaka kuongezeka Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman, ameeleza umuhimu kufanyika utafiti Zanzibar kuhusu ongezeko la talaka kutokana na kasi kubwa ya ndoa kuvunjika na athari yake ni kubwa.

Aliyasema hayo jana visiwani humo wakati akifunga kongamano la kikanda la wanasheria wanawake na watetezi wa haki za binadamu liloandaliwa na Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA).

Alisema moja ya kosa kubwa linalofanyika ni kufikiri wanandoa ni mke na mume na ndio maana watu wanashughulika kufundisha maisha ya ndoa wanaofunga ndoa pekee bila ya kujali wanaowazunguka.

"Mimi sijafanya utafiti, lakini niwashauri watakaofanya tafiti, moja ya kosa kubwa tunalolifanya katika eneo hili la ndoa ni kudhani wanandoa ni mke na mume tu. Wakati mkifanya tafiti mkinifuata naweza kuwaambia na mengine yanayosababisha wimbi la talaka," alisema Othman.

Aliishauri jumuiya ya wanasheria wanawake Zanzibar, kuweka mkazo maalumu katika utafiti wa masuala mbalimbali hasa tatizo linalojitokeza la kuvunjika kwa kasi kubwa ndoa hasa katika rika la vijana.

Pia, aliitaka ZAFELA kuongeza juhudi kwa kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa kuwa yapo makundi mengi yaliyo katika hatari ya kupoteza haki kutokana na kukosa msaada wa kisheria.

Aliitaka ijikite zaidi kuihamasisha jamii haki za wanawake na mambo ya kisheria yanayowahusu na kuzingatia haja ya ushiriki na ushirikishwaji katika masuala yote ya kidemokrasia.

Alisema ZAFELA ina nafasi ya kipekee ya kuiokoa taaluma ya sheria kutokana na kuporomoka kwa maadili hasa kwa vile wanawake wengi wana sauti ya kusaidia kuokoa dhidi ya ukosefu wa maadili ya taaluma hiyo.

Aidha, aliitaka jumuiya hiyo na nyingine kujenga mahusiano madhubuti ndani na nje ya nchi kwa kuwa kufanya hivyo ndio kutambulika na jumuiya kujiweka katika nafasi nzuri ya kujenga ushawishi wa kuaminika ndani ya jamii.

Mkuu wa Mkoa wa Mjini Mgharibi, Idrisa Kitwana Mustafa, alisema kuna umuhimu mkubwa wa kuwapo utafiti kuhusu ongezeko la talaka pamoja kufahamu chanzo cha tatizo hilo hasa kwa kuzingatia sababu za kuwapo hali hiyo hazijafahamika rasmi.

Alisema, upo umuhimu wa marekebisho ya sheria kuhusu suala hilo kuzingatia umakini wa kuifahamu kwa undani jamii kwa kuwa inawezekana ikasababisha madhara zaidi kwa vile wanaweza kujitokeza watu wakasababisha kuvunjika kwa ndoa kwa tamaa ya kupata mali.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma, Haroun Ali Suleiman, alisema moja ya sababu ya kuongezeka kwa wimbi la talaka ni wanaume kuoa mke zaidi ya mmoja na wanawake wengi hawapendi uke wenza.

"Nadhani utafiti huo tufanyiwe sisi wanaume kwanini tunatoa talaka sana, na sababu zipo nyingi na ofisi ya mufti tayari imeanza kutoa mafunzo ya ndoa baada ya kujua mambo yanayosababisha kuvunjika kwa ndoa, kweli tumepewa haki ya kuoa mke zaidi ya mmoja lakini hayo nayo yanasehemu yake tuyafikirie maana baadhi yao wanapoengeza mke mwengine humzarau mke wake wa kwanza," alisema.

Aidha, alisema serikali imefanya juhudi kubwa katika kuimarisha sekta ya sheria na kwamba hivi sasa ipo katika mchakato wa kukamilisha taratibu za kuanzisha mahakama malum ya udhalilishaji ikiwa ni jitihada za kupambana na tatizo hilo nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Jumuiya hiyo, Jamila Mahmoud Juma, alisema kongamano hilo limeaziimia kuwajengea uwezo wa elimu na kiuchumi jamii na wanasheria wanawake ili kujitegemea ikiwa ni hatua muhimu katika kupambana na vitendo vya udhalilishaji.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa CPS Africa, Sebastian Dietzold (kulia) na Mkurugenzi wa Maendeleo wa Mashariki ya Kati na Afrika Hilton Group, Sam Diab (kushoto) wakikabidhiana mkataba waliosaini wa kuanzisha mradi wa hoteli ya Canopy by Hilton The Burj Zanzibar unaotarajiwa kufunguliwa mwaka 2027 kwenye mji wa Fumba. Katikati ni Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Simai Mohammed Said. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# W'biashara, wawekezaji wahakikishiwa mazingira rafiki

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Idrissa Kitwana, amesema serikali itafanya kila iwezavyo kuhakikisha mazingira ya biashara, wafanyabiashara na wawekezaji unakuwa rafiki zaidi.

Aliyasema hayo visiwani hapa mwishoni mwa wiki wakati wa maadhimisho ya kilele cha sherehe za wiki ya shukrani kwa walipakodi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 maadhimisho ambayo yaliandaliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Kitwana katika maadhimisho hayo alimwakilisha Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Saada Salum Mkuya na kusema kuwa kila mmoja awajibike kulipa kodi kwa mujibu wa sheria.

Alisema TRA katika mwaka huo wa fedha imevuka malengo ya ukusanyaji kodi kwa asilimia 100.3 na kuipongeza kwa kazi nzuri kwa maslahi ya wananchi na taifa.

Aidha, alisema ukusanyaji huo umetokana na uadilifu wa wafanyakazi wake na kwamba ni vyema kuwajibika, kufuata maadili na kuwaongezea imani na ari wafanyabiashara ili kwenda sambamba na malengo ya serikali.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuongeza mapato ya nchi yatakayotumika katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo ikiwamo ujenzi wa barabara, shule, vituo vya afya na miundombinu ya majisafi na salama. Alisema wafanyabiashara ni wadau muhimu katika kuchangia maendeleo ya nchi kupitia kodi zao na kwamba ni vyema kulipa kodi kwa wakati kwa kutumia mifumo ya teknolojia.

Mkurugenzi wa Fedha kutoka TRA, Dina Edward, alisema kiwango hicho kikubwa cha ukusanyaji kodi ni matokeo ya kuwa na jamii ya walipa kodi wazalendo, waliohamasika na wenye kujitoa kwa dhati na kwa vitendo kuunga mkono juhudi za serikali kuliletea taifa maendeleo endelevu.

"Walipakodi hawa wamekuwa na mchango mkubwa bila ya kujali mazingira magumu ya kibiashara kwa baadhi ya chakati ambayo waliokuwa wakipitia kwa msingi huo napenda niwashukuru na kuwapongeza walipa kodi wetu," alisema.

Alisema katika mipango ya baadaye TRA imejipanga kuimarisha mifumo ya ulipaji wa kodi ili kuwarahisishia wafanyabiashara kufanya shughuli zao kwa urahisi.

Naibu Kamishna wa TRA Ofisi ya Zanzibar, Saleh Haji Pandu alisema kodi zote zinazokusanywa Zanzibar zinaingia katika mfuko wa hazina wa serikali ya Zanzibar kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Alisema kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022-2023 TRA ilipangiwa kukusanya Sh. tririoni 24.11 ambapo Zanzibar ilitakiwa kukusanya Sh. Bilioni 454.056 na kufanikiwa kukisanya Sh. 455.47, kiasi ambacho kimefanikiwa kuvuka malengo kwa asilimia 100.3.

Kaulimbiu ya maadhimisho ya kilele cha sherehe ya wiki ya mlipa kodi ni "Kodi yetu Maendeleo yetu, Tuwajibike".

# Wazalishaji, wauzaji vyakula mifugo wasiofuata taratibu kushughulikiwa

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi kupitia Wakala ya Maabara ya Veterinari nchini (TVLA), imetangaza kuwashughulikia wazalishaji na wauzaji wa vyakula vya mifugo wasiofuata sheria na kanuni zinazoongoza utekelezaji wa shughuli hizo.

Mtendaji Mkuu wa Wakala hiyo, Dk. Stella Bitanyi, alisema hayo mwishoni mwa wiki, alipokuwa akitoa taarifa fupi ya yaliyobainika wakati wa operesheni maalum iliyoendeshwa na timu ya wataalam kutoka ofisini kwake kwa kushirikiana na wakaguzi wa vyakula vya mifugo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ambao walifanya ukaguzi katika viwanda vinavyozalisha na maduka yanayouza vyakula hivyo katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, kuanzia Novemba 30 hadi Desemba mosi, 2023.

Dk. Bitanyi aliwataka wazalishaji wote wa vyakula vya mifugo nchini kuzalisha vyenye uwiano sahihi wa viinilishe vinavyohitajika kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa na mamlaka ya kuthibitisha ubora wa vyakula hivyo (TBS) na vya kimataifa kwa wale watakaohitaji kusafirisha nje ya nchi.

"Tunawaagiza kila kundi la chakula wanalozalisha wahakikishe sampuli yake inapelekwa kwenye maabara kuu ya veterinari ambao ndio wenye ithibati ya kitaifa ya kuchambua vyakula vya mifugo ili waweze kuthibitisha na kutoa vyeti vya ubora," alisema Dk. Bitanyi.

Aidha, aliwataka wazalishaji kupima malighafi zote wanazotumia kutengeneza vyakula vya mifugo na kuwaelekeza kusajili taasisi na mahali wanapozalishia vyakula hivyo.

"Tunafahamu kwamba usajili ni kila mwaka, ambao hawajasajiliwa wafanye hivyo na wale ambao tayari wameshasajiliwa waendelee kuhuisha usajili wao kupitia tovuti ya wizara ambako watapata maelekezo yote ya kufanya mazoezi hayo," alisema Dk. Bitanyi.

Akitoa malekezo upande wa wauzaji wa vyakula hivyo, Dk. Bitanyi aliwataka kununua vyakula vyao kutoka kwa wazalishaji waliothibitishwa kwenye viwango vya ubora kwa kila kundi la chakula wanalotaka kununua kwa wazalishaji hao.

Akizungumza na timu ya wataalam hao mmoja wa wazalishaji wa vyakula vya mifugo kutoka mkoani Pwani, Samson Maro, ameipongeza serikali kwa kufanya zoezi hilo mara kwa mara na kuahidi kuyafanyia kazi aliyoshauriwa na wataalam hao.

Mmoja wa wauzaji wa chanjo na vyakula vya kuku na bata kutoka mkoani humo, Domitila Melisa, amewaeleza wataalam hao namna anavyowasaidia wafugaji kwenye eneo lake kuwapa elimu na ushauri kuhusu aina ya chakula wanachopaswa kupewa ndege hao kulingana na umri walionao.

Akizungumzia hali yake ya ufugaji kabla ya kupewa elimu inayohusu vyakula vya mifugo, mfugaji wa kuku kutoka Kibaha, mkoani Pwani, Mwajuma Mwami, alisema alikuwa akinunua vifaranga na chakula cha kuku kwa kubahatisha jambo lililokuwa linasababisha vifo vya mara kwa mara vya vifaranga hao na kuiomba serikali kufanya ukaguzi na uhakiki wa viwanda na maduka ya vyakula vya mifugo kuwa endelevu.

Uzalishaji wa vyakula vya mifugo nchini unasimamiwa na Sheria ya Nyanda za malisho na chakula cha mifugo ya mwaka 2010 pamoja na kanuni zake zilizoandaliwa mwaka 2013, kwa pamoja vinawataka wazalishaji na wauzaji wa vyakula hivyo kuhakikisha wanyama wanapata vyakula bora ili waweze kuongeza uzalishaji wa mazao yao.



Mkurugenzi Mkuu wa Oryx Gas Tanzania Benoit Araman (katikati), Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake Tanzania( UWT), Marry Chatanda(wa pili kulia), Katibu Mkuu wa UWT, Jokate Mwegelo (wa tatu kulia),Waziri wa Nchi , Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambaye pia ni Mbunge wa Rufiji, Mohamed Mchengerwa (wa pili kushoto) wakimkabidhi mtungi wa Oryx na jiko lake mmoja wa Mama Lishe wa Wilaya ya Rufiji mkoani Pwani (wa tatu kushoto), lengo ni kuwawezesha Mama Lishe kutumia nishati safi ya kupikia badala ya kuni na mkaa.Wanaoshuhudia kushoto ni Meneja Masoko wa Oryx Peter Ndomba na kulia ni Mwenyekiti wa UWT Mkoa Pwani Zainab Vullu. Jumla ya mitungi 900 ya Oryx Gas na majiko yake yametolewa bure kwa Mama Lishe wote wa Wilaya hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali kushughulikia migogoro ya ardhi

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imesema inashughulikia migogoro yote mikubwa na midogo inayohusu ardhi ili imalizike kwa wakati kwa lengo la kulinda amani na utulivu nchini.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa kitengo cha Milki Kuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Dk. Upendo Matotola akisoma kwa niaba hotuba ya Naibu Waziri wa wizara hiyo, Geofrey Pinda, wakati wa uzinduzi wa ripoti ya haki za ardhi kwa wanawake nchini ambayo imeandaliwa na Shirika lisilo la kiserikali la Liberty Sparks.

Pinda alisema wapo baadhi ya watu wanaovamia na kujenga katika maeneo ya watu wengine kiholela jambo linaloendelea kutia mashaka.

"Serikali itaendelea kuhakikisha maeneo yote nchini yanapimwa na kutolewa hati za kisheria za umiliki ili kuhakikisha migogoro haitokei tena," alisema.

Alisema wizara inafahamu kuongezeka kwa makazi ya mijini na kupanuka kwa maeneo yanayokuwa kwa haraka kumeibua migogoro mingi mipya.

"Wizara inafahamu bado kuna changamoto, hasa katika masuala yanayohusiana na umiliki wa ardhi na mali kwa wanawake hapa nchini ambayo kwa sehemu kubwa imekuwa ikichochewa na mila, desturi na imani potofu za jamii za Watanzania na sheria zake azijafanywa rasmi," alisema Pinda.

Alisema serikali imeendelea kupitia utaratibu wa umilikishwaji wa ardhi na gharama zake ili kuwezesha Watanzania wote hasa masikini na vijijini kumiliki ardhi kihalali.

Akiwasilisha ripoti hiyo Mtafiti mshauri wa liberty sparks, Dk. Samweli Alananga, alisema utafiti huo ulilenga kujua hali za wanawake nchini na wamebaini licha ya sheria kuwa wazi kuhusu haki za wanawake tatizo kubwa lipo kwenye utekelezaji.

Dk. Alananga alisema chagamoto hizo zinachagiwa kwa kiwango kikubwa na mila, desturi na mazoea ambavyo zinasababisha mwanamke kushidwa kupewa kipaumbele.

"Eneo la urithi limeonekana watoto wa kike, wanawake wanapewa nafasi ya chini kulinganisha na watoto wa kiume," alisema.

Alisema ripoti hiyo imegusia serikali katika eneo la utawala na utatuzi wa migogoro ambalo imeonesha kuwa mingi imekuwa ikiwaathiri wanawake kuliko wanaume.

Alisema mfumo wa utatuzi wa migogoro umekuwa hautoi mazingira rafiki kwa wanawake wa kijijini kufikia mifumo ya utatuzi kutokana na chagamoto ya gharama.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Liberty Sparks, Evans Exaud, alisema linafanya utafiti katika maeneo yenye chagamoto ya migogoro ya ardhi.

"Ripoti hii imelenga kuhakikisha mwanamke anapiga hatua na kuwa chachu katika maendeleo ya nchi," alisema Exaud.

# Mbunge atoa msaada vitanda vya hospitali

**Na Steven William,** MUHEZA

NAIBU Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo na Mbunge wa Jimbo la Muheza, Hamisi Mwinjuma, amekabidhi vitanda na magodoro vinavyotarajiwa kuhudumia wagonjwa wa kwenye Hospitali ya Wilaya ya Muheza ya Samia Suluhu.

Mbunge huyo alikabidhi vitanda hivyo jana kwa Mganga Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Dk. Juma Mombokaleo, katika shughuli iliyofanyika hospitali ya wilaya na kuwashirikisha maofisa watendaji, kata na madiwani.

Alisema hayo ni matokeo ya mkakati wa hali ya utoaji wa huduma za afya kwa wananchi wa Wilaya ya Muheza huku akimshukuru Rais Samia Suluhu kwa kuleta fedha nyingi za ujenzi wa hospitali hiyo na vifaa.

Mwinjuma alisisitiza Ofisi ya Mganga Mkuu wa wilaya kuweka mfumo mzuri ili kuwarahisishia wananchi kupata huduma bora ya afya.

Alisema ni vizuri wilaya na hospitali zikajipanga na kuhakikisha dawa zote za msingi zinakuwapo kwa mujibu wa mwongozo kuondoa malalamiko.

Aliwapongeza watumishi wa hospitali ya wilaya na kuwataka kufanya kazi kwa kujitoa na kuwahudumia wananchi kwa lugha nzuri mbali na uchache wa watumishi walionao.

Dk. Mombokaleo alisema wamepokea vitanda 24 vyenye thamani ya Sh. milioni 16.

Alisema vitanda hivyo ni kwaajili ya uchunguzi wa magonjwa, kujifungulia na kulaza wagonjwa.

Alimshukuru Mbunge Mwinjuma kwa kuleta vitanda hivyo wakati mwafaka.

HABARI KITAIFA

# Mwalimu ailima barua CWT apinga bil. 7/- kufanya sherehe

**Na Mwandishi Wetu**

MWALIMU Victor Kazoba amekiandikia barua Chama cha Walimu Tanzania (CWT), kwenda kwa Katibu Mkuu wa chama hicho, Japhet Maganga, akipinga maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani na kumbukizi ya miaka 30 ya chama hicho kwa kutoa hoja nane.

Nipashe ilimtafuta mwalimu huyo aliyeko Halmashauri ya Muleba baada ya kuona barua iliyoandikwa Desemba mosi, mwaka huu iliyokuwa na saini yake na kuthibitisha kuwa ni yake na nakala kwenda kwa Rais Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu, Katibu Mkuu Wizara ya Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu na Rais wa CWT, Leah Ulaya.

Katika barua hiyo, mwalimu huyo mwenye namba CWT.KGR/MLB.577 alisema hoja zake ni kwamba tarehe ya maadhimisho ya siku ya mwalimu duniani ni Oktoba 5, ambayo duniani kote inaadhimishwa, na kwamba chama hicho kikiwa sehemu ya wataalam na wasomi kufanya tofauti na siku iliyopitishwa kimataifa ni kuitweza taaluma ya ualimu.

"Aibu hii haiwezi kuwa ya walimu pekee bali kwa taifa zima na Tanzania."

Hoja ya pili, ni kiwango kikubwa cha bajeti kilichopangwa kutumika katika sherere hizo kinachokadiriwa kuwa zaidi ya Shilingi bilioni saba.

"Matumizi ya namna hii yanapelekea chama kuingia kwenye mikopo katika taasisi za fedha pasipo sababu ya lazima kufanya hivyo."

Mwalimu Victor alisema kuadhimisha kumbukizi ya miaka 30 ya kuanzishwa kwa CWT kwa kutumia kituo kimoja cha Jiji la Mwanza na kuacha miji mingine yote haina shughuli yoyote, hakuna tija.

Alisema ni vyema hata kuingia maadhimisho ya taasisi zingine mfano Chama Cha Mapinduzi ambako maadhimisho yake hufanyika kwa kila tawi, wilaya, mkoa na hivyo kila mwanachama kuhusika na pakiwa na ujumbe mahususi na kuleta tija ya maadhimisho kwa wanachama wote ambao ndiyo walengwa.

Hoja nyingine ni kufanyika kwa sherere hizo wakati watumishi wa CWT wakiwa na madai yao ambayo hayajalipwa hadi sasa yahusuyo stahiki mbalimbali kama uhamisho, likizo, matibabu, misiba na malimbikizo ya michango na tozo katika mifuko ya hifadhi ya jamii ya NSSF na PSSSF.

Hoja nyingine ni kushindwa kuendeleza miradi ya ujenzi wa ofisi ya chama ngazi ya wilaya ulioanzishwa na ofisi kwa kupewa ruzuku na ofisi makao makuu.

"Kitendo cha kusitisha uendelezaji wa miradi hiyo yenye tija kwa walimu moja kwa moja na fedha kutumika katika matumizi ya starehe inatafsirika kama matumizi mabaya ya fedha za chama," alisema.

Hoja nyingine aliyoitoa ni kukosekana kwa elimu kwa wanachama wenye kuelimishwa mambo mbalimbali yahusuyo stahiki zao katika utumishi kwasababu za kukosekana fedha wakati zinapangiwa matumizi ya sherehe ni matumizi mabaya ya fedha za wanachama.

Hoja nyingine ni uwepo wa deni kubwa la malipo ya mkono wa kwaheri kwa walimu wanachama wa CWT waliostaafu kwa kipindi cha mwaka 2018 hadi 2023.

Kadhalika katika hoja ya nane amesema ni uwapo wa deni kubwa la mawakili waliotoa huduma ya utetezi kwa walimu wanachama wa CWT na kuna ushahidi wa wadai kushtaki chama mahakamani kudai haki zao, jambo ambalo ni fedheha kubwa kwa taasisi inayotetea maslahi ya watumishi.

"Sababu hizo chache zimenifanya kukuandikia barua wewe Comrade Katibu wa chama, ufanye maamuzi magumu ya kusitisha sherehe hizo...," alisema katika barua hiyo ya kurasa mbili.

Nipashe ilimtafuta Katibu wa CAT Taifa, Maganga, alijibu kwa mkato; "Sipo tayari kukusikiliza".

Mwandishi alipomshi kutaka kusikiliza upande wake, alishikilia msimamo wake na kukata simu.

Nipashe ilimtafuta Rais wa CWT Taifa, Leah ambaye alisikiliza hoja zote nane na kusema; "Mwambie huyo mwalimu arudi kwenye wilaya yake atapata majibu yote. Huko alikopeleka barua hatasaidiwa arudi wilayani kwake."



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kulia) akimpatia cheti Meneja Mwandamizi wa Afya, Usalama na Mazingira wa GGML, Dk. Kiva Mvungi kutambua mchango wa kampuni hiyo katika Mfuko wa Udhamini wa Ukimwi (ATF) kuisaidia serikali kuendeleza mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika kitaifa mkoani Morogoro mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watu 49 wauawa na wanyama hifadhini

**Na Jenifer Gilla**

SERIKALI imebainisha kuwa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi 2021, wananchi 49 kwenye Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA), walipoteza maisha kwa kuliwa na wanyama wakali, huku wengine wakijeruhiwa na kuisababishia mamlaka kutumia gharama kubwa kuwatibu.

Kutokana na hali hiyo, serikali imesema haitotumia nguvu kuwahamisha wananchi wanaoishi katika eneo hilo kwenda maeneo mengine, bali itatoa elimu na ushawishi ili waone tofauti ya maisha ndani ya NCAA na maeneo yaliyoandaliwa Msomera, wilayani Handeni mkoani Tanga.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi alisema wananchi hao hawawezi kufanya shughuli za maendeleo kutokana na masharti ya kuishi ndani ya hifadhi, hali inayosababisha maisha yao kuzidi kuwa duni.

"Kwahiyo, wakati Watanzania wengine wanapewa fursa za shughuli za kiuchumi, mikopo, wanajengewa huduma za kijamii na miundombinu, wale wa ndani ya hifadhi haiwezekani. Maisha yao yameendelea kuwa duni wakiishi kwa kupatiwa msaada wa vyakula na NCAA," alisema.

**Kwahiyo, wakati Watanzania wengine wanapewa fursa za shughuli za kiuchumi, mikopo, wanajengewa huduma za kijamii na miundombinu, wale wa ndani ya hifadhi haiwezekani.**

Matinyi alitaja changamoto nyingine ni kuwa maisha ya wananchi hao kuendelea kuwa hatarini kadri wanavyozidi kuongezeka kwa kuwa wanasogea zaidi kwa wanyama wakali na kusababisha baadhi yao kudhuriwa au kuuliwa.

Alisema kuwapo watu hao hifadhini pia kunaathiri shughuli za uhifadhi na utalii kwa kuwa wageni wanapoinga katika hifadhi hiyo, asilimia 44 ya eneo wanakutana na binadamu na mifugo, huku baadhi ya wanyamapori wakilazimika kuhama.

Alikumbusha kuwa mwaka 1959 wakati hiyo inaanzishwa, ilikuwa na wakazi 8,000 na mifugo michache, lakini sasa idadi imeongezeka na kufikia watu 115,000 na mifugo zaidi ya 806,000, wakichukua kilomita za mraba 3,700, sawa na asilimia 44 ya eneo lote la hifadhi.

Matinyi alisema kutokana na hali hiyo, serikali iliamua kuwaandalia maeneo salama na rafiki kwao, ili wapate huduma muhimu za kijamii na fursa za kufanya shughuli za maendeleo ikiwamo mikopo.

Alisema katika awamu ya kwanza walijenga nyumba 503 katika Kijiji cha Msomera, Wilaya ya Handeni mkoani Tanga ambazo zilihamia kaya 551 zenye jumla ya wananchi 3,010 na mifugo 25,521.

Katika awamu ya pili ya mradi huo, Matinyi alisema wanatarajia kujenga nyumba 5,000 katika vijiji vya Msomera nyumba 2,500, Saunyi nyumba 1,000 na Kitwai wilayani ya Simanjiro nyumba 1,500.

Alisema katika awamu hiyo, wanatarajia kuhamisha kaya 10,000 na mpaka sasa kaya 500 zimeshajiandikisha kuhama kwa hiari na 406 zimeshafanyiwa uhakiki.

Alisema ukiacha kupewa nyumba kubwa yenye vyumba ya kulala vitatu ndani ya eneo la ekari mbili na nusu, wananchi hao pia wanapewa shamba lenye ukubwa wa ekari tano, eneo la kuweka mifugo kwa wafugaji na kujengewa mabwawa na visima vya maji ya kutumia na kunyweshea mifugo.

Alisema maeneo hayo pia yanajengewa barabara, mifumo ya umeme, visima vya maji, minada ya kisasa na vituo vya kuuza maziwa kwa wafugaji.

Alisema wananchi hao wana uhuru wa kuhamia eneo lolote nchini na wale watakaoamua kuishi nje ya eneo waliloandaliwa, watapata fidia ya Sh. milioni 15 iwasaidie katika makazi yao mapya.

Aprili 6, 2021, Rais Samia Suluhu Hassan alitoa angalizo kwa Wizara ya Maliasili na Utalii na NCAA kuhusu kasi hiyo ya ongezeko la watu hifadhini, akiwataka waangalie uwezekano wa kuiokoa hifadhi hiyo iliyokuwa imeelewa na idadi kubwa ya watu na mifugo na kuathiri shughuli za utalii.

Juni mwaka 2022, serikali ilianza kuwahamisha kwa hiyari wananchi waliokuwa tayari kwenda nje ya hifadhi kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kutishia uhai wa eneo hilo muhimu kwa utalii nchini.

# UMOJA CUP RORYA 2023 ROBO FAINALI KUANZA KUPIGWA KESHO

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya mtifuano mkali ulioanza mwanzoni mwa mwezi uliopita, hatimaye mashindano ya soka ya kila mwaka wilayani Rorya, maarufu Umoja Cup, yamefikia hatua ya robo fainali, ambayo itaanza kupigwa rasmi kesho, Jumanne.

Timu nane zilizofanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo ambayo lengo lake mbali na kutoa burudani kwa Wanarorya, ni kuibua vipaji na kujenga umoja na ushirikiano wilayani humo, ni KMT ya Sota itakayocheza na Kabwana fc ya Mkoma, Shirati Mji ya Mkoma itakayocheza na Kyariko ya Raranya.

Nyingine ni wenyeji, Wanamaji FC ya Sota itakayovaana na Mafundi fc, pamoja na Bubombi ya Bukura Mpakani itakayokuwa na shughuli pevu dhidi ya Gonga fc kutoka Nyamongo.

**Robo fainali ya kwanza hapo kesho itawakutanisha Vijana wa KMT dhidi ya Kabwana fc wakati ya pili kati ya Shirati Mji Fc na Kyariko Fc ikitarajiwa kuchezwa Alhamisi wiki hii, mechi zote zikipigwa Uwanja wa Maji Shirati Sota.**

Akizungumzia michuano hiyo ya Umoja Cup Rorya 2023, Meneja wa Mashindano, Danile Maina, alisema yamekuwa ya mwendelezo na yanazidi kukua kila mwaka jambo ambalo wanamshukuru mdhamini wao kwa, Peter Owino, kwa juhudi kubwa anazofanya kuhakikisha yanafanyika kila mwaka.

"Mdhamini wetu anajitahidi kuhakikisha kila mwaka mashindano haya hayakwami ili wadau wa soka wilayani Rorya waendelee kupata burudani na vijana waendeleze vipaji vyao", alisema Maina.

Kuhusu kupatikana mshindi aliyestahili kutokana na uwezo wake uwanjani, Maina alisema mashindano hayo yanayodhaminiwa na mdau wa michezo wilayani Rorya, Owino, huchezeshwa na waamuzi makini kutoka mkoani Mara.

Maina alizitaja zawadi zitakazotolewa kwa washindi wa Umoja Cup 2023; mshindi wa kwanza mbali ya medali na kombe ataondoka na Sh. 500,000, wa pili atajinyakulia Sh. 150,000 na seti moja ya jezi, huku wa tatu akizawadiwa seti moja ya jezi na Sh. 50,000 na mshindi wa nne akibeba mpira Sh. 30,000.

"Kocha bora wa mashindano, atazawadiwa 'tracksuit', huku mchezaji bora akiondoka na Sh. 20,000 sawa na mfungaji bora na kipa bora ambaye mbali na kiasi hicho cha fedha atapewa pia zawadi ya 'gloves', wakati mchezaji chipukizi akiondoka na kiatu. Timu yenye nidhamu itazawadiwa 'jozi 15 za 'stocking' (soksi za kuchezea mpira)," alisema.

Timu zilizoshiriki mashindano hayo yalikuwa yakichezwa kwa mfumo wa mtoano (nyumbani na ugenini), kabla ya kutinga hatua ya robo fainali ni Kirengo fc, Wanamaji fc ambao ni wenyeji, KMT fc, Masonga, Bubombi, Victoria, Kirongwe, Donga, Nyahera, Kabwana United, Homeboys, Shirati Mji, Kyariko, Rifa, Wimbi na Mafundi fc ambao ni mabingwa watetezi.



Kikosi cha Wanamaji FC ya Sota, kitakachovaana na Mafundi FC katika hatua ya robo fainali ya michuano ya Umoja Cup Rorya 2023 inayoendelea wilayani humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Azam kuhamishia dozi Ligi Kuu FA Cup*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Azam FC imesema dozi za mabao mengi inazotoa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kwa sasa, itazihamishia kwenye Kombe la Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), maarufu Kombe la FA.

Klabu hiyo imetoa onyo hilo juzi siku chache baada ya ratiba ya raundi ya pili ya Kombe la FA kutoka, huku Azam ikipangwa kucheza na Alliance ya Mwanza katika mechi ambazo zimepangwa kuchezwa Desemba 15 hadi 17.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hasheem Ibwe, amesema baada ya kutoka kwa ratiba hiyo, wameanza kujipanga kikamilifu ili kutwaa Kombe kwa sababu wana historia nzuri, pia ni kombe ambalo wana bahati nalo.

"Tunaamini kwamba hili kwanza ni kombe ambalo tumekuwa na wakati mzuri sana nalo, huwa tuna bahati nalo, na timu tunayokwenda kucheza nayo imeshawahi kucheza Ligi Kuu, na kama inavyojua msingi wa timu hiyo ni vijana wa akademi, siyo wa kununua huku na huku, au nje ya nchi, ni wale ambao unawatengeneza wenyewe kutoka shule, hivyo hauwezi kuwa mchezo rahisi.

"Lakini niwaambie tu mashabiki wa Azam, vipigo vinavyotokea huku kwenye Ligi Kuu sasa vitahamia Kombe la FA, dozi ni ile ile, hatuna upendeleo, sindano iliyoshona koti ndiyo itashona ngozi," alitamba Ibwe.

Kwa siku za karibuni, Azam FC imekuwa ikitoa vikigo vikubwa katika mechi za Ligi Kuu, mara ya mwisho ikiikandika Mtibwa Sugar mabao 5-0, Novemba 24, lakini kabla ya hapo iliizichapa Mashujaa FC 3-0, mechi ikipigwa Novemba Mosi na ikaifumua Ihefu SC 3-1, Novemba 4 mwaka huu.

Msimu uliopita Azam ilitinga fainali ya kombe hilo, ikalikosa kwa kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Yanga, mechi ikichezwa Juni 12 mwaka jana, Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, lililowekwa wavuni na Mzambia Kennedy Musonda.

## Bares ategemea dirisha dogo kuibeba Mashujaa

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mashujaa FC, Abdallah Mohamed 'Bares' (pichani chini), amekiri kuwa na kipindi kigumu kwa sasa, lakini akifurahia kuona dirisha dogo la usajili likiwadia, jambo ambalo atakwenda kulitumia vema kuimarisha safu yake ya ushambuliaji, ambayo imekuwa na mapungufu kadha wa kadha kwenye mbio za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na Nipashe jana, Bares alisema ameona makosa ya kikosi chake ikiwamo kushindwa kutengeneza nafasi nyingi na kufunga mabao kwenye michezo yao.

Alisema katika michezo iliyopita hakuwa na matokeo mazuri ukiwamo juzi ambao walikubali kichapo cha mabao 3-2 dhidi ya KMC FC, tatizo kubwa limekuwa kushindwa kuzitumia nafasi chache wanazotengezeza.

"Tutaongeza nguvu dirisha dogo kwa kusajili watu wa kushambulia maana huko tumekuwa tuna shida, pia tutaangalia safu ya ulinzi na viungo, kwa sababu ya kufanya vizuri katika michezo iliyopo mbele yetu," alisema Bares.

Aliongeza kuwa licha ya kutopata matokeo mazuri katika michezo miwili iliyopita, bado hawajaondoka katika mipango yao ya kuhakikisha wanamaliza kwenye nafasi ya saba katika msimamo wa ligi hiyo.

Bares alieleza bado wapo kwenye mapambano ya kutafuta matokeo chanya kwenye michezo iliyopo mbele yao, akiendelea kuwahimiza wachezaji kuwa makini ikiwamo safu ya ushambuliaji kwa kipindi ambacho dirisha la usajili bado halijafunguliwa.

Alisema kuwa kwa sasa akili na nguvu zao wanazielekeza katika mechi ijayo watakayokuwa nyumbani dhidi ya Tabora United kuhakikisha wanavuna alama muhimu katika mchezo huo utakaopigwa kesho kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma.



## ZISIKUPITE

### VIGOGO EPL KWA TAYLOR

KLABU za Tottenham Hotspur, Aston Villa, Newcastle United na Brighton zipo kwenye mbio moja na Manchester City na Manchester United kumuwania kiungo wa kati wa Uholanzi, Kenneth Taylor mwenye umri wa miaka 21 kutoka Ajax. ***(Teamtalk)***

### MESSI AJAYE ATAKIWA CITY

MANCHESTER City inamfuatilia chipukizi wa Argentina, Claudio Echeverri, huku kiungo mshambuliaji huyo wa River Plate mwenye umri wa miaka 17, akitajwa kama Lionel Messi ajaye. ***(Mirror)***

### LEWANDOWSKI KUACHWA

BARCELONA inaweza kumwachia mshambuliaji wa Poland, Robert Lewandowski kama mchezaji huru mwishoni mwa msimu wa 2024-25 kwa sababu ya kipengele katika mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35. ***(Sport via Sun)***

### PHILLIPS NA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inamfuatilia kiungo wa kati wa Manchester City, Kalvin Phillips, 28, kabla ya dirisha la uhamisho la Januari. ***(Football Insider)***

### ALONSO KURUDISHWA REAL

KLABU ya Real Madrid inataka kumchukua kiungo wake wa zamani, Xabi Alonso ili arudi Bernabeu kuwa kocha kutoka kule Bayer Leverkusen. ***(Mirror)***

### MAIGNAN AWANIWA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich inaweza kujitosa kumsajili mlinda mlango wa AC Milan, Mike Maignan, 28, kuchukua nafasi ya Mjerumani Manuel Neuer, 37. ***(Sky Germany)***

### ZERBI MKATABA MPYA

KOCHA wa Brighton, Roberto de Zerbi, huenda akabaki katika klabu hiyo huku wakijiandaa kumpa mkataba mpya baada ya taarifa za kutakiwa Manchester United. ***(Football Insider)***

### CARRICK ASAKA NYOTA

KOCHA wa Middlesbrough, Michael Carrick, anataka kuongeza wachezaji katika dirisha la majira ya baridi, huku nyota wa Nottingham Forest, Joe Worrall, 26 na Charlie Cresswell (21), kutoka Leeds United wakiwa miongoni mwa walengwa. ***(Sun)***

### THURAM AWANIWA LIVER

KLABU ya Liverpool inapania kumleta kiungo wa kati wa Nice na Ufaransa, Khephren Thuram mwenye umri wa miaka 22, pale Anfield. ***(Fichajes)***

### BOBB KUFUNGWA UPYA

KLABU ya Manchester City inakaribia kufikia mwafaka wa kumpa mkataba mpya, mshambuliaji wa Norway, Oscar Bobb, 20. ***(90 min)***

### WILLIAMS NA BARCELONA

BARCELONA haitalipa ada ya euro milioni 50 iliyowekwa kwenye kifungu cha kutolewa katika mkataba mpya wa mshambuliaji wa Athletic Bilbao, Nico Williams, 21, katika hatua ambayo inampa mchezaji huyo fursa ya kujiunga na klabu zingine msimu ujao. ***(Mundo Deportivo)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# HISPANIA KATIKA KUNDI LA KIFO MICHUANO EURO 2024

**NYON,** Uswisi

DROO ya michuano ya Euro 2024 ya majira ya joto yajayo nchini Ujerumani imefanyika na kushuhudia Ufaransa na Hispania zikiwekwa kwenye kundi la kifo.

**Jumla ya timu 21 tayari zimefuzu kwa michuano hiyo, huku nafasi tatu zaidi zikiwa bado na zitapatikana baada ya mechi za mchujo zitakazochezwa Machi mwakani.**

Ufaransa imepangwa Kundi D, ambapo itamenyana na Uholanzi, Austria na washindi wa Playoff A (kati ya Poland, Wales, Finland na Estonia).

Kikosi hicho cha kocha, Didier Deschamps ambacho kilibeba Kombe la Dunia mwaka 2018 na kufika fainali mwaka 2022, kinatarajia kufanya marekebisho kwenye michuano ya euro iliyopita, ambapo walitolewa katika hatua ya 16-bora.

Hispania ambayo ilishinda michuano hiyo mwaka 2008 na 2012, imepangwa Kundi B, ambapo itakabiliwa na mtihani mgumu baada ya kupangwa dhidi ya Mabingwa Watetezi, Italia na Croatia waliofika nusu fainali Kombe la Dunia 2022 na Albania.

**Kocha England naye ahofu, asema timu zote wanazocheza nazo ni zaidi ya...**

England bado wanatafuta taji lao kuu la kwanza la wanaume tangu mwaka 1966, ilimaliza nafasi ya pili baada ya kushindwa kwa mikwaju ya penalti na Italia katika michuano ya mwaka 2021 na vijana hao wa kocha Gareth Southgate wamepangwa Kundi C pamoja na Denmark, Slovenia na Serbia.

"Siku zote unahisi upo kwenye karatasi," alisema Southgate akiwaambia waandishi wa habari baada ya droo ya makundi hayo.

"Timu zote tunazocheza ni zaidi ya uwezo. Nilikuwa nimetulia kwa yote hayo. Unajua lengo ni kuondoka kwenye kundi."

Ujerumani imekuwa katika hali mbaya mwaka huu, ipo Kundi A pamoja na Scotland, Hungary na Uswisi.

Michuano hiyo itaanza Juni 14, huku fainali zikipangwa kwenye Uwanja wa Olympia mjini Berlin Julai 14, 2024.

**Makundi kamilia euro 2024:**

Kundi A: Ujerumani (wenyeji), Scotland, Hungary, Uswisi, huku Kundi B likiundwa na Hispania, Croatia, Italia na Albania.

Kundi C ni Slovenia, Denmark, Serbia na England, wakati Kundi D ni mshindi wa mchujo A, (Poland/Wales/Finland/Estonia), Uholanzi, Austria na Ufaransa.

Kundi E ni Ubelgiji, Slovakia, Romania, mshindi wa Mchujo B (Israel/Bosnia/Ukraine/Iceland) na Kundi F ni Uturuki, mshindi wa mchujo C (Georgia/Ugiriki/Kazakhstan/Luxembourg), Ureno na Jamhuri ya Czech.

# ODEGAARD ATAKA UBORA ZAIDI ARSENAL




**LONDON,** England

MARTIN Odegaard amekiri Arsenal inahitaji kuimarika zaidi baada ya kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Wolves, Jumamosi.

Wenyeji walipata faida ya mabao 2-0 pale kwenye Uwanja wa Emirates, huku Bukayo Saka na Odegaard kila mmoja akifunga bao ndani ya dakika 15.

Hata hivyo, 'Washikabunduki' hao waliwaruhusu Wolves kurejea mchezoni wakati walipofunga bao zikiwa zimesalia dakika nne za muda wa kawaida.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway, Odegaard amesisitiza kuwa Arsenal lazima wafanye vizuri zaidi wanapokuwa kwenye uongozi bora.

Nahodha huyo mwenye umri wa miaka 24, alisema: "Tulianza tena kwa nguvu sana. Kipindi cha kwanza kilikuwa kizuri. Tulifunga mabao mawili mazuri na kutawala kila kitu.

"Tumewaruhusu waingie kidogo tukiwa na bao, lakini huo ni mpira wa miguu. Nadhani tunapaswa kujifunza kutokana na hilo.

"Tunajua kwenye Ligi Kuu huwezi kamwe kuzima mchezo. Leo ulikuwa mfano mzuri wa hilo. Lazima tuhakikishe tunafanya vema zaidi wakati ujao tukiwa 2-0."

Lakini licha ya kukosolewa kwa kukosa umakini, Odegaard alifurahishwa na kiwango cha Arsenal.

Aliongeza: "Imekuwa wiki nzuri na matokeo mazuri. Tupo kileleni na lazima tuzidi kuimarika na kuendelea kusonga mbele.

"Ratiba ni ngumu, lakini karibu msimu mzima ni mgumu. Huna muda mwingi wa kupona.

"Lazima tuwe wajanja katika kupona na kupumzika kabla ya mchezo unaofuata dhidi ya Luton."

Ushindi dhidi ya Wolves unamaanisha kuwa Arsenal wako kileleni mwa jedwali mwa msimamo kwa pointi nne, huku safari ya kuelekea Luton ikitarajiwa Jumanne.

# Kocha Newcastle amsifu Gordon

**NEWCASTLE,** England

KOCHA Eddie Howe anafurahi kuona Anthony Gordon akipata kutambuliwa kwa kustahili baada ya mchango mzuri wakati akiiwezesha Newcastle United kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Manchester United, Jumamosi.

Winga huyo mwenye umri wa miaka 22 alifunga bao muhimu lililofanikisha ushindi huo na kuwafanya Magpies hao kujivuta hadi nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu England.

Gordon alipiga krosi iliyoongozwa kwa ustadi kutoka kwa Kieran Tripper katika dakika ya 55 na kuzua shangwe kwenye uwanja wa St James' Park.

Mchezaji huyo wa zamani wa Everton sasa amefunga mabao sita ya ligi kuu msimu huu - na Howe alimsifia nyota huyo aliyesajiliwa kwa pauni milioni 45.


Alisema: "Tangu siku ya kwanza alipofika kwenye klabu hii, uliona shauku aliyokuwa nayo na nia yake ya kutaka mafanikio zaidi.

"Anawaza mazoezi kila siku na wakati mwingine tunalazimika kwenda kumtoa nje ya uwanja wa mazoezi.

"Kakabiliana na beki mzuri sana leo (juzi) Aaron Wan-Bissaka, lakini yeye alikuwa bora zaidi kimwili. Ilikuwa vita nzuri sana kati yao wawili.

"Nimefurahi kuwa anafunga mabao sasa na kupata kutambuliwa anakostahili."

Howe alilazimika kuanzisha kikosi kilichotoka sare ya bao 1-1 na Paris Saint-Germain dhidi ya United kutokana na tatizo la majeraha linaloendelea, huku kipa Nick Pope akipata tatizo la bega mwishoni mwa kipindi cha pili.






# *Rashford atakiwa kuungwa mkono*

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, amesema Marcus Rashford atapata "uungwaji mkono" katika jitihada za kurudisha upya kiwango chake baada ya kutokuwa na wakati mzuri wakati wakifungwa na Newcastle.

Man United ilipoteza kwa bao 1-0 kwenye Uwanja wa St James' Park Jumamosi huku Rashford akitolewa baada ya dakika 61.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa England alifunga mabao 30 katika michuano yote msimu uliopita, lakini amefanikiwa kufunga mabao mawili pekee katika mechi 18 msimu huu.

"Najua hili suala linakuja na Marcus anawekeza sana, tunamuunga mkono na atarudi kwenye kiwango chake," alisema Ten Hag.

"Anafanya kazi kwa bidii na anajituma sana. Atarejea, atapona na atapata msaada wetu wote."

United sasa wamepoteza mechi sita za Ligi Kuu England msimu huu na 10 katika mashindano yote.

Walipiga shuti moja tu lililolenga lango dhidi ya Newcastle huku vijana wa kocha Eddie Howe wakirekodi majaribio 22, likiwamo la mpira wa adhabu wa Kieran Trippier uliogonga mwamba wa goli.

## HABARI MICHEZO

# TWIGA STARS NA DK. 90 ZA MWISHO KUFUZU WAFCON

Na Saada Akida

ZIKIWA zimebaki dakika 90 tu kabla ya kujihakikishia tiketi ya kwenda fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wanawake (WAFCON), mwakani nchini Morocco, Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Tanzania, Bakari Shime, amesema kazi kubwa anayoifanya ni kuwajenga kisaikolojia wachezaji wake ili kuwapunguzia mzigo wa mawazo kichwani.

Amesema wachezaji wanaweza kuwa wanawaza kuwa tayari wameshafuzu kutokana na ushindi wa mabao 3-0 walioupata kwenye mechi ya awali nchini, hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo katika mechi ya marudiano.

**Akizungumza na Nipashe jana, Shime alisema ameona mapungufu ya kikosi chake na ubora wa wapinzani wao, Togo ambao wanatumia nguvu pamoja na kufika langoni mwa mpinzani mara nyingi.**

Alisema mwisho na dakika 90 za mchezo wa kwanza nyumbani ni maandalizi ya mechi yao ya marudiano dhidi ya Togo ambayo wanahitaji kuzuia kutoruhusu bao au kuendelea kushinda ugenini.

Shime alisema atahakikisha kwanza safu ya ulinzi inakuwa makini katika mchezo wao wa marudiano ambao wanaenda kucheza ugenini na muhimu ni kushinda ili kwenda kucheza fainali hizo.

"Tumeshinda nyumbani mabao 3-0 hii ni faida kwetu, lakini hatutakiwi kujisahau na kuona tumeshafanikiwa kucheza fainali, tunajipanga vizuri kufanyia kazi mapungufu yetu na ubora wa Togo ili twende tukatafute matokeo chanya ugenini na kujihakikisha kwenda katika fainali hizo," alisema Shime.

Aliongeza kuwa anaamini kama wachezaji wake watafuata maelekezo anayowapa uwanja wa mazoezi watafanikiwa kushinda mechi hiyo ya marudiano na kupata nafasi ya kucheza fainali za Wafcon mwakani.

Kikosi cha Twiga Stars kiliondoka jana kuelekea nchini Togo kwa ajili ya kukamilisha dakika 90 za mchezo wa marudahia dhidi wenyeji wao hao utakaochezwa kesho. Tanzania inahitaji sare au ushindi wowote ili kucheza fainali baada ya mechi ya kwanza kushinda mabao 3-0 katika mechi iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam.




Mshambuliaji wa Yanga na mfungaji wa bao pekee wakati wakitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Al Ahly, Pacome Zouzoua, akipasua ngome ya wapinzani wao hao kwenye mechi ya Kundi D ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Gamondi akubali kwa Al Ahly sasa aipania Medeama

INATOKA UKURASA 24

kushinda ugenini," alisema Gamondi.

Aliongeza kuwa wanaenda katika uwanja wa mazoezi kufanyia kazi mapungufu yao na kupigania alama tatu za ugenini dhidi ya Medeama FC, kwani wakishinda watajiweka kwenye nafasi nzuri ya kusaka tiketi ya kwenda robo fainali.

Kocha Mkuu wa Al Ahly, Marcel Koller (pichani), alisema kipindi cha kwanza mechi ilikuwa ya ushindani mkubwa na walitengeneza nafasi na kushindwa kuzitumia ipasvyo.

Alisema kipindi cha pili waliingia na mpango mwingine na kufanikiwa kupata bao la kuongoza kabla ya Yanga kuchomoa na kufanya matokeo kuwa bao 1-1.

"Kwa matokeo ya sare ugenini si mbaya, kubwa ni kuendelea kujiandaa kwa mechi yetu ijayo kuhakikisha tunaendelea kusaka ushindi," alisema Koller.

Kwa matokeo hayo, Al Ahly inaongoza Kundi D ikiwa na alama nne ikifuatiwa na Medeama yenye pointi tatu sawa na CR Belouizdad huku Yanga ikiendelea kuburuza mkia kwa alama yake moja.



## *Mbeya City sasa yazidi kupotea Championship*

Na Adam Fungamwango

DALILI za Mbeya City kurejea Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kuteremka msimu uliopita zinazidi kufifia baada ya juzi kupokea kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Mbuni FC, mchezo uliopigwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha.

Mabao ya Mbuni yalifungwa na beki wa zamani wa Simba, Paul Bukaba kwa mkwaju wa penalti, akimfunga kipa wa zamani wa timu hiyo ya mtaa wa Msimbazi, Jeremiah Kisubi, bao la pili likiwekwa wavuni na Baraka Mwangosi, Adili Buha akifunga bao pakee kwa Mbeya City.

Baada ya matokeo hayo, Mbeya City, iliyopanda na kucheza Ligi Kuu msimu wa 2013/14, kabla ya kushuka 2022/23, imeporomoka hadi nafasi ya nane ikiwa na pointi 18 kwa michezo 13 iliyocheza mpaka sasa.

Timu ya Ruvu Shooting nayo imejiweka katika mazingira mazuri ya kucheza Ligi Daraja Pili 'first league' msimu ujao baada ya kukubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Cosmopolitan kwenye Uwanja wa Jamhuri, Dodoma.

Hicho ni kipigo cha 12 kwa timu hiyo iliyoshuka daraja msimu uliopita kutoka Ligi Kuu, ikiwa ndiyo timu pekee ambayo haijashinda mechi yoyote ikitoka sare moja tu, ikiwa imeshacheza mechi 13 mpaka sasa.

Kwenye Uwanja wa Sokoine Mbeya, vinara KenGold yenye maskani yake jijiji Mbeya, walizidi kuweka hai matumaini yao ya kucheza Ligi Kuu msimu ujao baada ya kuitandika TMA mabao 2-0.

Ushindi huo umeiwezesha KenGold kufikisha pointi 29 na kuiacha TMA kwenye nafasi yake ya tatu na pointi zake 26.

Kabla ya mechi hiyo iliyochezwa Uwanja wa Sokoine, Mbeya, timu zote mbili zilikuwa na pointi 26.

Kwenye Uwanja wa Jamhuri, Morogoro, Transit Camp ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Stand United.

## Benchikha atoa sababu

INATOKA UKURASA 24

inakihitaji, walituacha sisi tumiliki mpira na wakawa wanatushambulia kwa kushtukiza, mpango wao ulikuwa mzuri, wana wachezaji wazuri pia, ila naweza kusema mpaka sasa kundi bado liko wazi, tutakwenda kuwekana sawa ili tuangalie mechi zijazo tunachezaje," alisema kocha huyo.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally alisema pamoja na kukosa matokeo ya ushindi, lakini kwa mara ya kwanza timu yao imecheza kwa kiwango kikubwa chini ya kocha Benchikha.

"Si matokeo mabaya sana na wala si mazuri ya kujivunia, tulikuwa na nafasi kubwa ya kupata ushindi, nadhani katika mechi zote tulizocheza msimu huu za mshindano yote, leo (juzi) ndiyo tumecheza kwa kiwango cha juu sana.

"Timu inatia matumanini hasa baada ya ujio wa mwalimu, kinachotufanya tusiwe na tabasamu ni kukosa tu ushindi lakini si kiwango," alisema Ahmed.

Kwa matokeo hayo, Simba inashika nafasi ya tatu kwenye Kundi B, ikiwa na pointi mbili mpaka sasa na bao moja, baada ya juzi usiku Asec Mimosas kuifunga Wydad bao 1-0, hivyo Waivory Coast hao wanaongoza kwa pointi nne na mabao mawili, Jwaneng Galaxy ikishika nafasi ya pili kwa pointi nne na bao moja, huku Wydad ikishika mkia ikiwa haina pointi wala bao.

Michezo
Jumatatu Desemba 4, 2023
Nipashe



Odegaard ataka ubora zaidi UKURASA 22

# Gamondi akubali kwa Al Ahly sasa aipania Medeama



Na Saada Akida

●●● Auchambua mchezo huku akieleza...

BAADA ya kupata sare kwa mbinde dhidi ya Al Ahly ya Misri kwenye mechi ya hatua ya makundi iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema hajaridhishwa na matokeo hayo, hivyo sasa ameamua kuufungia kazi mchezo ujao dhidi ya Medeama ya Ghana.

**Yanga juzi usiku walilazimisha sare ya bao 1-1 dhidi ya Al Ahly ya Misri, matokeo ambayo yanaiweka katika mazingira magumu ya kwenda hatua ya robo fainali ya michuano hiyo, ingawa nafasi bado ipo kama wakianza kupata ushindi.**

Akizungumza na Nipashe jana, Gamondi alisema mechi ilikuwa ya vipindi viwili, dakika 45 ya kipindi cha kwanza walicheza vizuri na kutengeneza nafasi na kushindwa kuzitumia, lakini kipindi cha pili wapinzani wao, Al Ahly waliingia kwa mpango mwingine na kuushika mchezo.

Alisema Al Ahly walifanikiwa kuingiza watu wenye spidi, kipindi cha pili ambao waliwavuruga, na kukiri kuwa hawakucheza vizuri licha ya kupata bao la kusawazisha, lakini pamoja na hayo wanapaswa kusahau matokeo hayo na kuangalia mechi iliyopo mbele yao.

"Mechi ilikuwa ya ushindani mkubwa, Al Ahly wamefanikiwa katika mipango yao, sasa tunarejea uwanja wa mazoezi kusahihisha makosa yetu kuelekea mchezo ujao dhidi ya Medeama FC.

"Mchezo huo ni muhimu kwetu kushinda ili kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kufikia malengo yetu ya kucheza robo fainali, tunatakiwa kupambana

INAENDELEA UKURASA 23



# Benchikha atoa sababu Simba kukosa ushindi Botswana

Na Adam Fungamwango

KOCHA Mkuu wa Simba, Mualgeria Abdelhak Benchikha, amesema wachezaji wake kutokuwa na kasi, hasa mita 30 kabla ya kulifikia lango la wapinzani wao, ndicho kilichowanyima ushindi kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa hatua ya makundi iliyochezwa juzi dhidi ya Jwaneng Galaxy, Uwanja wa Obed Itani Chilume, jijini Francistown, Botswana.

Akizungumza baada ya mechi hiyo kutamatika kwa suluhu, Benchikha alisema wachezaji wake hasa washambuliaji na viungo wake hawakuwa na kasi wanapolikaribia lango la mpinzani wao, hivyo kuwapa urahisi mabeki wa timu pinzani kuokoa na kusoma mienendo yao.

"Ilikuwa mechi nzuri kiukweli, tumekosa pointi tatu licha ya kucheza vizuri. Mita 30 kabla ya lango la Jwaneng Galaxy hatukucheza kwa kasi ya kushambulia na tumepoteza mabao mengi kutokana na kutokuwa na ufanisi, sijui kama niwe na furaha au nisiwe nayo kwa sababu pointi moja sifikiri kama ni nzuri kwetu, hasa baada ya mechi iliyopita dhidi ya Asec Mimosas," alisema kocha huyo aliyekuwa akiiongoza Simba kwa mara ya kwanza.

Kocha huyo aliwasifu wapinzani wao kutokana na mpango mkakati walioingia nao uwanjani, wakiwaachia mpira, wakikaa nyuma na kushambulia kwa kushtukiza.

"Tumepoteza pointi mbili nyumbani na leo tumepoteza pointi mbili ugenini, ila mwisho kabisa nasema sipendezwi na hali hii.

"Jwaneng Galaxy ni timu nzuri inayoonyesha nini

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >